epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Mei 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581677
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA 22

SOUTHGATE APATA KIGUGUMIZI HATIMA YAKE ENGLAND

# Kicheko Sekta Mifugo, Uvuvi

UKURASA 2



**Waziri atamba na maono ya R4 za Samia**

**Fungu laongezwa hadi bilioni 460/-**

**Meli, boti za kisasa za uvuvi na vizimba kuinua uchumi zaja**

**Chanjo za mifugo kufungua masoko zaidi nyama ya Tanzania ughaibuni**

**Ndege maalum kudhibiti uvuvi haramu**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, bungeni Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 5

**MADAKTARI AFYA AKILI WAKOSHWA REKODI MPYA YA BAJETI YAO**





UKURASA WA 18

**CHADEMA YAKAMIA JIMBO LA CHATO KWA HALI NA MALI**

UKURASA WA 19

**MHARIRI MTENDAJI NIPASHE ATWAA TUZO KIMATAIFA**



## Ajali ya lori, Noah yaua watu saba

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza katika Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika, jijini Paris, Ufaransa jana. **PICHA: IKULU**

MKUTANO NISHATI PARIS

## Mwenyekiti Samia aibuka na vikwazo vinne Afrika

UK.3

**MICHEZO** GAMONDI AANIKA SIRI UBINGWA 2023/24 UK.24

**KATUNI** UK.6



Wachuuzi wa fedha wakiwa wamezipanga wakati wakisubiri wateja ambao asilimia kubwa ni makondakta wa daladala katika kituo cha mabasi cha Makumbusho, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. Noti ya 1,000/- inauzwa kwa 700/- hadi 800/-. **PICHA: JOHN BADI**

# Ajali ya lori, Noah yaua saba

**Na Ashton Balaigwa**, MOROGORO

WATU saba wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa baada ya gari dogo la abiria aina ya Toyota Noah walilokuwa wakisafiria kutoka Kilosa kwenda Morogoro Mjini kugongana uso kwa uso na lori katika eneo la Dakawa, wilayani Mvomero, barabara kuu ya Morogoro - Dodoma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Alex Mkama, alisema kuwa ajali hiyo ilitokea jana majira ya saa 2:30 asubuhi.

Mkama alisema gari dogo la abiria lilikuwa likitokea mji mdogo wa Dumila wilayani Kilosa kwenda Morogoro mjini wakati lori hilo la masafa marefu lilikuwa linatokea Morogoro Mjini kwenda Dodoma.

Aliyataja magari yaliyohusika na ajali kuwa ni Tayota Noah lenye namba za usajili T 101 DKB na lori aina ya MAN lenye namba za usajili RS 980 X3 na kwamba yalikuwa yakisafiri katika uelekeo tofauti. Watu sita walifariki dunia papo hapo.

Mkama alisema ajali hiyo ilitokea baada ya lori hilo kuacha njia likiwa limeyapita magari mengine na kukutana uso kwa uso na gari dogo la abiria na kusababisha vifo hivyo na wengine kadhaa kujeruhiwa.

Alisema baada ya kutokea ajali hiyo, dereva wa lori alitoweka eneo la tukio na kukimbia huku akilitelekeza gari hilo na polisi wanaendelea kumsaka.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mvomero, Dk. Francis Paul, alisema saa 2:30 asubuhi, walipata taarifa ya kutokea kwa ajali eneo la Dakawa wilayani humo na baadaye kidogo, waliwapokea majeruhi saba na miili ya watu sita waliofariki dunia kwenye eneo la tukio.

Dk. Paul alisema majeruhi hao saba, kati yao wawili walikuwa kwenye hali mbaya na walisafirishwa kwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya matibabu zaidi lakini mmoja alifariki dunia akiwa njiani.

"Mpaka sasa, watu waliofariki dunia ni saba na majeruhi ni sita na waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mvomero hali zao si mbaya kwani hawajapata majeraha makubwa bali ni mshtuko na majeruhi madogo madogo na watapata tiba hapa kwetu," alisema Dk. Paul.

Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo, Maimuna Salum, mkazi wa Dumila, alisema walipofika eneo la Bwawa la Hatari karibu na mji wa Dakawa, aliona mbele yake gari aina ya lori lilitokea Morogoro likiwa linataka kuyapita magari yaliyo mbele na gari lao likiwa karibu na kugongana uso kwa uso.

"Nilikaa nyuma ya kiti cha mbele kwa dereva na tuliobahatika kutoka ni kama watatu hivi na wengine waliokuwa mahututi walipelekwa hospitali kubwa ya mkoa wa Morogoro na wengine wamefariki dunia, akiwamo dereva wa gari letu," alisema.

# Kicheko sekta mifugo, uvuvi

**Na Romana Mallya**

MENO ya wadau wa sekta za mifugo na uvuvi nchini 'yatakuwa nje' katika mwaka ujao wa fedha ikiwa mikakati iliyowekwa na wizara yenye dhamana nazo itatekelezwa.

Wizara hiyo imepanga, pamoja na mambo mengine, kununua meli nne za uvuvi Bahari Kuu na nyingine kwa ajili ya mafunzo ya uvuvi pamoja na boti 450 na zana za uvuvi. Pia kununua maboya 60 na ndege saba zisizo na rubani kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu nchini.

Hayo ni miongoni mwa yaliyoelezwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipowasilisha bungeni jana kusoma makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2024/25, akiomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 460.333 kwa ajili ya wizara hiyo.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 97.215 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 363.118 ni kwa ajili ya maradi ya maendeleo. Fungu la wizara hiyo limeongezeka kutoka Sh. bilioni 298.921 za mwaka huu wa fedha (2023/24).

Ulega alisema kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, watafanya kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo kwa kutoa chanjo kwa magojwa 13 ya kipaumbele na kuboresha na kuendeleza hekta 20,000 za maeneo ya malisho.

Alisema hatua hiyo inalenga kufungua masoko zaidi ya nyama ya mifugo na mazao yake nje ya nchi.

Ulega alisema ili sekta ya mifugo na uvuvi ipate mafanikio ni lazima uchumi uwe jumuishi kwenye mazingira ambayo migogoro baina ya wakulima, wafugaji na wadau wengine kwenye mnyororo wa thamani inapunguzwa au kuondolewa kabisa.

"Bajeti imezingatia falsafa ya R4 za Rais Samia Suluhu Hassan, inayolenga kwenye maridhiano, uhimilivu, mageuzi na kujenga uchumi imara na ujumishi. Kwa mipango tuliyoweka na kupanga kuitimiza katika bajeti hii, nina uhakika R4 za Rais zitakuwa na faida kubwa kwenye mifugo na uvuvi," alisema Ulega.

Katika sekta ya uvuvi, Waziri Ulega alisema wanakusudia kuandika alichokiita "Historia ya Samia Suluhu Hassan", akiwa na ufafanuzi kwamba ni Rais shupavu atakayemaliza kadhia ya uvuvi haramu kwa kuweka na kutekeleza mikakati madhubuti ya muda mfupi, wa kati na mrefu.

Alitaja moja ya mikakati yao ni kutumia teknolojia za kisasa kudhibiti uhalifu wa uvuvi katika bahari na maziwa. Watatumia ndege maalum zisizokuwa na rubani (drones) zenye uwezo wa kusafiri kilomita 100 kwa saa mbili na kuchukua picha za kiwango cha juu za uhalifu wa uvuvi haramu na utoroshaji mazao ya uvuvi.

Waziri Ulega aliitaja ni hatua itakayoongeza ufanisi na kupunguza matumizi ya rasilimali fedha na muda huku wizara ikikusudia kuanza kutumia mfumo wa ufuatiliaji kielektroniki ambao utafungwa katika vyombo vyote vya uvuvi zikiwamo boti za kisasa zilizotolewa hivi karibuni.

"Mfumo huu utafuatilia mienendo yote ya wavuvi nchini ikiwamo kuweka kumbukumbu za mavuvi, utasaidia kuweka usalama wa wavuvi na wananchi ambao wanapata matatizo wakiwa maeneo ya maji," alisema Ulega.

Alieleza kuwa kwa mwaka 2024/25, miradi na shughuli zitakazotekelezwa katika sekta ya mifugo ni pamoja na kuanza kutekeleza Mradi wa Mageuzi katika Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (T-CSDTP) wa miaka mitano, ukinufaisha walengwa 58,000.

Mradi huo unahusisha ng'ombe wa maziwa 17,200; kujenga mabanda 5,000 ya ng'ombe na kujenga mfumo wa uvunaji maji ya mvua katika kaya 22,400.

Waziri huyo pia alisema watanunua na kusanikisha mitambo 2,800 ya biogesi; kujenga vituo 950 vya kukusanya maziwa; kununua dozi 929,000 za chanjo za mifugo na kujenga kilomita 140 za barabara.

"Pia tutanunua na kusambaza madume 60 ya mbari bora za mifugo aina ya Brahman ili kuongeza uzalishaji na tija katika mnyororo wa thamani wa mifugo na mazao yake," alisema.

Waziri Ulega pia alisema watajenga kituo cha mafunzo ya wadau wa mnyororo wa thamani wa malisho aina ya mabingobingo (Juncao); wataboresha na kuendeleza hekta 20,000 za maeneo ya malisho katika eneo la Msomera, Kitwai na Saunyi na kukamilisha ujenzi wa mabwawa saba na visima virefu vitatu.

Alisema watawezesha uendeshaji mashamba ya kuzalisha malisho na mbegu za malisho; kuwezesha mradi wa Maziwa Faida TALIRI Tanga na African Dairy Genetic Gain katika mikoa saba na kuiwezesha TALIRI na TAFIRI kufanya utafiti.

Ulega pia alisema wizara imepanga kuanzisha kambi moja ya mifugo wageni katika Ranchi ya Mkata kupitia mpango wa vitalu vilivyoboreshwa kwa kuwekewa miundombinu muhimu ya ufugaji ikiwa ni pamoja na malisho, maji na huduma za ugani, lengo ni kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Pia alisema wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi itapima na kuweka mipaka eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta 500,000 kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Waziri huyo alibainisha kuwa hadi Aprili mwaka huu, jumla ya ng'ombe 2,957,724 na mbuzi/kondoo 2,828,248, wenye thamani ya Sh. trilioni 3.4, waliuzwa katika minada nchini kulinganishwa na ng'ombe 2,218,293, mbuzi/kondoo 2,121,187 wenye thamani ya Sh. trilioni 1.7 waliouzwa mwaka 2022/23.

Vilevile, hadi kufikia Aprili mwaka huu, jumla ya tani 13,745.38 (zikiwamo tani 1,024.33 za nyama ya ng'ombe, tani 9,982.67 za mbuzi, tani 3,195.09 za kondoo, tani 32.35 za kuku na tani 10.94 za nguruwe zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 56.6), zimeuzwa nje ya nchi kulinganishwa na tani 12,243.8 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 51.9 kwa mwaka 2022/23. Hilo ni ongezeko la asilimia 12.3.

Alisema kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu, Sekta ya Uvuvi imezalisha jumla ya tani 472,579.34 za mazao ya uvuvi na kati yake, tani 429,168.39 zilivunwa kwenye maji ya asili na tani 43,410.95 ni kutoka ukuzaji viumbe maji. Kufuatia uzalishaji huo, jumla ya tani 41,271.07 za mazao ya uvuvi na samaki hai 134,572 wa mapambo ziliuzwa nje ya nchi.

Waziri Ulega pia alisema kuwa hadi kufikia Aprili, 2024 wizara ilikuwa imetoa vibali 44 vya kuingiza chakula kutoka nje ya nchi kwa kampuni 15 na kuwezesha kampuni hizo kupata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa forodha.

***SOMA HOTUBA YA WAZIRI ULEGA UK. 9-14**

## HABARI KITAIFA

# Samia ataja vikwazo vinne nishati safi

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja mambo manne yanayokwamisha juhudi za upatikanaji wa nishati safi ya kupikia Afrika, ambayo yanatakiwa kutatuliwa ili kufikia lengo la dunia la kuondoa hewa ukaa.

Samia aliyasema hayo jana wakati akihutubia mkutano wa kwanza wa nishati safi ya kupikia jijini Paris, Ufaransa, uliowakutanisha takribani wawakilishi 1,000 kutoka karibu nchi 50.

Mkutano huo unafanyika wakati matumizi ya nishati isiyo salama katika kupikia yakishika kasi.

Kwa mujibu wa Wakala wa Nishati wa Kimataifa (IEA), watu bilioni 2.3 kutoka nchi 128 duniani wanavuta hewa chafu kwa kutumia njia isiyo salama kupikia, ikiwamo mkaa.

Mkutano huo pamoja na mambo mengine, utajadili namna ya kusaidia mabilioni ya watu kubadilisha mfumo wa kupika ambao unazalisha hewa hatari kwa afya na kupunguza vifo zaidi ya milioni vinavyotokea kabla ya wakati, vingi vikiwa katika bara la Afrika.

Alisema kutokana na ukosefu wa upatikanaji wa nishati safi na endelevu ya kupikia kwa bei nafuu, kaya nyingi hususan vijijini, zinapata ugumu wa kuitumia. Alitaja sababu kubwa kuwa ni gharama kubwa, upatikanaji mdogo na minyororo duni ya ugavi.

Rais Samia alitaja sababu nyingine kuwa ni ufadhili hafifu na ukosefu wa uelewa kuhusu fursa za kiuchumi katika suala hilo, huku maendeleo ya upatikanaji wa suluhisho yakiwa yamezuiwa na ukosefu wa utafiti na ubunifu wa kutosha.

Sababu ya tatu, kwa mujibu wa Samia, ni ukosefu wa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa wote. Alisema kikwazo kingine kipo kwenye kuzipatia suluhisho changamoto hizo, akieleza kuwa msisitizo lazima uwekwe kwenye kutambua suluhisho linalowezekana na nafuu.



Alisema Afrika yenye kiwango cha juu zaidi cha ongezeko la watu na rasilimali zote muhimu, linashika nafasi ya chini katika upatikanaji wa nishati safi ya kupikia hali inayowaweka watu wake katika hatari kiafya.

"Zaidi ya Waafrika milioni 900 wanategemea masuluhisho yasiyo safi ya nishati ya kupikia ambayo huchangia katika uharibifu wa mazingira, kupoteza baianowai na hatari za kiafya," alisema.

Kwa mujibu wa IEA, kutumia nishati safi wakati wa kupikia kama vile gesi au umeme kutaokoa uzalishwaji wa tani 1.5 za hewa chafu ifikapo mwaka 2030.

Alisema kwa kuzitambua changamoto hizo, Tanzania hivi karibuni ilizindua Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia wa miaka 10 wenye lengo la kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati mbadala ya kupikia kufikia 2034.

Pia alisema mkakati huo unadhamiria kuanzisha mfuko wa kitaifa ili kusaidia upatikanaji wa nishati safi ya kupikia na Waziri Mkuu atausimamia kwa hali ya juu ili kulinda afya za watumiaji na kuokoa mazingira. Samia alisema kutumia nishati safi kupikia, kunaondoa athari chanya kwa watumiaji katika nchi zao, dunia na mazingira kwa jumla hivyo basi ni muhimu ajenda hiyo kuwa kipaumbele kwa Afrika.

Alilipongeza IEA kwa kutangaza mwaka 2024 kuwa mwaka wa kupika kwa nishati safi na kwa kuitisha mkutano huo, na wote waliohudhuria na kujadili ili kuhakikisha nishati safi kwa wote inapatikana.

Kwa mujibu wa Rais Samia, ajenda ya nishati safi ya kupikia barani Afrika ikipewa msukumo itasaidia kutunza mazingira kwa kuongeza maendeleo ya vijana na kuwapa wanawake fursa zaidi ya kushiriki shughuli zingine za maendeleo na uzalishaji na hivyo kupunguza umaskini na ukosefu wa usawa.

Alisema ili kufikia ajenda hiyo kunahitajika mifumo ya msaada na sera zinazotoa mwongozo wa kupatikana kwa nishati hiyo kwa bei nafuu na teknolojia kote barani. Alisema ili kufikia lengo la kifedha ambalo IEA imekadiria ili kupatikana nishati safi kwa wote ifikapo mwaka 2030 mkutano huo unapaswa kuelekeza maombi ya ufadhili kwa wadau kama vile Mfuko wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Waziri Mkuu wa Norway, Jonas Støre, alisema maboresho ya nishati ya kupikia yatapunguza uzalishwaji wa hewa chafu, kuboresha afya na kuunda fursa za ukuaji wa kiuchumi.

"Norway ni mfuasi thabiti wa kupika kwa nishati safi, na nimefurahi kutangaza leo kwamba tumejitolea kuwekeza takriban dola milioni 50 katika sababu hii muhimu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa IEA, Fatih Birol, alisema dola bilioni 2.2 zilizopatikana katika mkutano huo ni mwanzo nzuri wa safari ya kutokomeza matumizi nishati isiyosalama kupikia na kusaidia upatikanaji wa haki za msingi kama vile afya bora, usawa wa kijinsia na elimu.

Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Akinwumi Adesina, alisema kwa kushirikiana na nchi mbalimbali wameongeza ufadhili katika kusukuma ajenda ya nishati safi kupikia hadi dola milioni 200 kila mwaka kwa muongo mmoja ujao, kupitia Mfuko wa Nishati Endelevu kwa Afrika (SEFA).


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende "pay via mobile". Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# CAF: Watazamaji wapate chakula, vinywaji katika Uwanja wa Mkapa

• Serikali yataja inachovuna, profesa aonesha mbinu za kuongeza mapato

**Na Sanula Athanas**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF) limeagiza Uwanja wa Benjamin Mkapa unaokarabatiwa, uwe na huduma ya chakula na vinywaji kwenye majukwaa yote.

Hii itawezesha watazamaji kujinunulia wanachotaka kula au kunywa huku wakifuatilia mchezo uwanjani.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Habari na Masoko wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Boniface Wambura, hivi sasa huduma ya chakula na vinywaji uwanjani hapo inatolewa kwenye Jukwaa la Watu Mashuhuri (VVIP) pekee.

Ofisa Usalama wa Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA) nchini, Inspekta Hashim Abdallah, katika ufafanuzi wake kwa mwandishi wa habari hizi, anasema CAF imetoa maelekezo hayo baada ya timu yake ya wataalamu kukagua uwanja huo na kubaini hauna huduma hiyo kwa watazamaji.

Anasema wataalamu wa CAF walitua nchini mwezi Machi mwaka huu kukagua Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam na Uwanja wa Amaan, Zanzibar ili vitumike wakati wa mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) yaliyopangwa kufanyika nchini Septemba mwaka huu.

"CAF wameelekeza kwamba kuanzia msimu ujao, viwanja vyote vinavyotumika kwenye mashindano yao, viwe na huduma ya chakula na vinywaji kwa ajili ya watazamaji," anasema.

Inspekta Abdallah anaeleza kuwa CAF pia imeelekeza mechi za mashindano inayosimamia zisichezwe kwenye uwanja ambao hauna viti kwa ajili ya watazamaji.

Kwa mujibu wa Wambura, aliyekuwa sehemu ya timu ya wakaguzi wa CAF, msimu ujao wa soka (2024/25) utaanza Agosti mwaka huu.

Wambura anaeleza kuwa hivi sasa, kwa mechi za ngazi ya klabu, kanuni za mashindano za TFF zinaelekeza timu mwenyeji kugharamia huduma za chakula na vinywaji kwa ajili ya VVIP. Kwa mechi za timu za taifa, TFF inagharamia chakula na vinywaji kwa ajili ya kundi hilo (VVIP).

Maelekezo hayo ya CAF yanatoa fursa kwa watazamaji kujinunulia vitafunwa na vinywaji vitakavyouzwa uwanjani. Ni fursa ya soko la bidhaa kama biskuti, bisi, sambusa, korosho, soda, juisi na maji.

Kifungu cha 8(6) cha Kanuni za Usalama za FIFA kinaelekeza, "maeneo yote ya uwanja yafikike kwa urahisi na kuwapo vibanda maalum vya kupata viburudisho (vitafunwa na vinywaji) uwanjani."



Moja ya ndoa zilizofungwa kwenye uwanja wa Nou Camp mwaka 2022. Uwanja wa Benjamin Mkapa unaweza kuingiza mamilioni kupitia utaratibu huu.

**UTALII WA MICHEZO**

Wakati CAF ikielekeza hayo, Tanzania hivi sasa ina utalii wa michezo. Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa anasema Uwanja wa Benjamin Mkapa ni nguzo ya kuvuna fedha za kigeni.

Hilo linaungwa mkono na Meneja wa uwanja huo, Milinde Mahona, anayeelezea mikakati inayotekelezwa mahali hapo; wakivuna Sh. milioni 905 mwaka 2022/23 na katika mwaka huu wa fedha, wanatarajia kukusanya Sh. milioni 907 kutokana na mapato ya uwanja huo.

Hata hivyo, wenye taaluma yao ya uchumi wanasema "hizo hazitoshi." Prof. Aldin Mutembei wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) anataja njia tano zinazoweza kuongeza mapato ya uwanja huo. Huyu ni msomi wa taasisi mpya ya kitaaluma chuoni hapo inayoitwa 'Confucius Institute', inayojikita katika mwingiliano wa kitaaluma kati ya China na Tanzania.

Hiyo inajumuisha uhusiano wa lugha ulioingia hadi masomoni hivi sasa, utamaduni, diplomasia ya uchumi na biashara.

Meneja wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Mahona, anasema mkakati wao ni kuanzisha rasmi utalii michezo baada ya kukamilisha maboresho yanayoendelea uwanjani.

Hiyo ina maana ya kuzinduliwa rasmi 'hifadhi mpya ya utalii', ikiungana na ubunifu mwingine katika sekta ya afya ambako hivi sasa kuna utalii tiba, hata leo kuna wageni walioingia nchini kutoka Sierra Leone kwa ajili ya utalii huo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, wamepokea timu ya wataalamu wa Wizara ya Afya ya Sierra Leone, wakiongozwa na Mganga Mkuu wa nchi hiyo, Sertie Kenneh. Wameingia makubaliano JKCI kutibu wagonjwa wanaotoka Sierra Leone.

Meneja Mahona anasema Uwanja wa Benjamin Mkapa una utalii wa ndani unaohusisha mambo kadhaa; shule na vyuo hupeleka wanafunzi kutembelea mahali hapo kujifunza pasi na kulipia gharama yoyote mithili ya darasa la Makumbusho ya Taifa.

"Wanafunzi wanapotembelea uwanjani hujifunza mambo mbalimbali ya michezo, lakini uwanja wenyewe ni utalii tosha. Ninaamini kwamba siku zijazo utakuwa utalii mkubwa zaidi," Mahona anasema.

Ni hoja ambayo Prof. Mutembei anaitafsiri kwamba, "wanafunzi wakitoka hapo, wanakuwa mawakala wa kutangaza uwanja huo na bidhaa zake."

Kuhusu michezo ya kimataifa kwenye uwanja huo, Meneja Mahona anasema ujio wa watazamaji na wanamichezo kwa ajili ya michuano husika unakaribisha watalii wa kigeni.

Anasema kuwa kwa kutumia saikolojia ya utalii, ujio wa wageni hao nchini - viongozi, wanamichezo na mashabiki wao ni fursa kubwa kiuchumi. Wanakusanya mapato ya mlangoni huku wageni wakiondoka na mengi ya mvuto yatokanayo na maisha ya Kitanzania na vivutio vya utalii vilivyopo.

Meneja huyo anataja baadhi ya vivutio hivyo ni vyakula vya asili, lugha ya Kiswahili, hifadhi za taifa na utamaduni wa Kitanzania. Wanasafiri kurudi kwao wakiwa na hisia za kurudi tena nchini kuja kufaidi mazuri yaliyowakosha.

"Klabu Bingwa Afrika msimu huu, mechi za robo fainali, una-

## KUHUSU UWANJA WA MKAPA

**Watu 70,000** waliingia Uwanja wa Mkapa, Oktoba 26, 2008 kutazama mechi ya kwanza ya watani wa jadi, Simba na Yanga.

**Sh bil 1.67** mapato yaliyopatikana kutokana na mechi ya kirafiki kati ya Taifa Stars na Brazil iliyochezwa Juni 7,2010 rekodi ambayo bado haijavunjwa.

**Sh mil 900** wastani wa mapato ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa mwaka.

**Sh bil 31** gharama za maboresho ya Uwanja wa Benjamin Mkapa.



## RIPOTI YA UCHUNGUZI



Sherehe nyingine ya harusi iliyofanyika Nou Camp 2022.

zungumzia mechi mbili; Simba dhidi ya Al Ahly na Yanga dhidi ya Mamelodi Sundowns. Hatua ya makundi ya Klabu Bingwa Afrika unazungumzia mechi sita.

"Kuna mechi za Timu ya Taifa ya Soka (Taifa Stars). Hizo timu ngeni zinakuja na mashabiki wake. Timu inakuwa na wachezaji 30 hadi 35, ukijumlisha na benchi la ufundi, watafika watu 50 hivi. Kuna timu zinakuja na mashabiki hadi 500, hivyo wanakuja watu wengi nchini," anasema.

Meneja huyo anaeleza kuwa wageni hao hufikia hotelini, ambako huona vivutio mbalimbali vya utalii kama vile picha za hifadhi za taifa.

"Kwahiyo, kupitia michezo tunapata wageni wengi sana kutoka nchi mbalimbali. Uwanja huu una vitu vingi; kuna viwanja vya michezo mbalimbali, kuna kumbi za mikutano na sherehe, kuna maeneo ya wazi ambayo yanatumika kwa shughuli mbalimbali kama vile harusi na matamasha," anasema.

Mahona anasema uwanja huo una viwanja vya michezo mingine kama vile mpira wa mikono, mpira wa kikapu na mpira wa wavu. Pia una chumba cha mazoezi (gym).

"Kuna viwanja vya ndani ambapo mashindano mpaka ya Kanda ya Tano ya Mpira wa Kikapu huwa yanafanyika; timu za Rwanda, Misri, Burundi, DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) zinakuja kucheza hapa," Mahona anaeleza.

Mkakati wa kuongeza mapato wa Meneja Mahona unafanyiwa uchambuzi wa kitaalamu na Prof. Mutembei anayesema kumbi za mikutano za Uwanja wa Mkapa ni fursa kubwa ya kuupa soko uwanja huo.

Prof. Mutembei ambaye ni mbobevu pia katika masuala ya diplomasia ya uchumi, utafiti, elimu na mawasiliano, anasema kufanya sherehe kwenye uwanja huo kunaipa hadhi sherehe yenyewe, hivyo ni fursa kibiashara kwa wasimamizi wa uwanja huo.

"Dar es Salaam kwa sasa ina kumbi nyingi kwa ajili ya sherehe. Kinachopaswa kufanywa na menejimenti ya Uwanja wa Mkapa ni kuangalia bei za washindani, kisha wao wanashusha kidogo. Mfano, kama kumbi zingine wanatoza Sh. 500,000 kwa siku, wao watoze Sh. 400,000 au Sh. 450,000 kwa siku," Prof. Mutembei anasema.

Msomi huyo anasema mkakati huo ukitekelezwa, na wasimamizi wa uwanja wakaweka udhibiti mzuri wa mapato, kuna fursa kubwa Uwanja wa Mkapa kuwa kitegauchumi kinachoaminika serikalini.

Marejeo hai ya mkakati wa aina hiyo kwenye kitegauchumi, yako katika klabu ya soka ya Barcelona ya Hispania. Juni 2022 ilipoyumba kiuchumi, iliruhusu uwanja wake wa Nou Camp kutumika kuingiza fedha kwa shughuli tofauti na soka.

Hiyo inajumuisha sherehe za harusi na hafla zingine za kijamii. Kutokana na umaarufu wa uwanja huo, uliwezesha tozo kubwa, mfano Euro 1,600 (Sh. milioni 4.4) kwa sherehe ya harusi.

Mapato ya sasa ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ya wastani wa Sh. milioni 900 kwa mwaka, ni sawa na Sh. milioni 75 kwa mwezi au Sh. milioni 2.5 kwa siku. Hizo ni Sh. 104,000 kwa saa au Sh. 1,700 kwa dakika.

Prof. Mutembei anataja mbinu ya kuwapo mabonanza ya michezo uwanjani hapo, akiwa shahidi wa soko kwa kinachofanyika Viwanja vya Leaders Club, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam.

Hata hivyo, Prof. Mutembei anatoa angalizo, washiriki wa mabonanza hayo wasiingie eneo la kiwanja cha soka ili kulinda ubora wake. Eneo hilo analitaja "ndiyo mtaji namba moja wa Uwanja wa Mkapa", hoja inayoungwa mkono na Meneja Mahona.

Prof. Mutembei anataja eneo lingine la burudani linalokosha umma ni muziki, akisema Uwanja wa Benjamin Mkapa ni mahali sahihi pa kutekeleza mialiko ya wanamuziki maarufu wa kigeni na wazawa.

"Wasimamizi wa uwanja wakumbuke kilichokuwa kinafanywa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Vipindi na Uzalishaji wa Clouds Media Group, Ruge Mutahaba (alifariki dunia Februari 26, 2019).

"Kwa kushirikiana na viongozi wenzake wa vyombo hivyo vya habari, waliandaa matamasha hayo kwa mafanikio makubwa, wakiwaleta nchini wasanii maarufu kutoka DRC, Uganda na kwingineko ulimwenguni," Prof. Mutembei anasema.

Vilevile, msomi huyo anashauri uongozi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa kuendeleza kanuni kongwe ya masoko - matangazo mbalimbali ya uwanja kwenye vyombo vya habari na kutumia watu maarufu kunadi mradi huo ili ujumbe na yanayoendana na uwanja huo yaufikie umma.

Katibu Mkuu Msigwa anataja hatua walizopiga katika kuingiza Uwanja wa Mkapa sokoni, mojawapo ni Timu ya Taifa ya Soka Uganda (Cranes) kuweka kambi nchini na kutumia uwanja huo kwa mechi za kuwania kufuzu kushiriki Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Botswana (Juni 3, mwaka huu) na Algeria (Juni 10, mwaka huu).

Anasema hatua hiyo ni fursa ya kuingiza watalii na fedha za kigeni nchini, pia kutangaza nchi na vivutio vyake vya utalii. Sasa vivutio vya Tanzania vitatangazwa na timu za taifa za Algeria, Botswana na Uganda kupitia uwanja huo.

Msigwa pia anaunga mkono kauli ya Meneja Mahona kwamba timu zinapoingia nchini zinakuja na makundi ya watu, ambao hufikia hotelini, wanaleta fedha za kigeni na wizara yake hulipwa uwanja unapotumika.

Kimsingi, hoja ya kuboresha huduma za Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuongeza mapato iliibuliwa miaka 13 iliyopita na Kamati Maalum ya Kudhibiti na Kuboresha Mapato ya TFF.

Kamati hiyo ilitoa ripoti yake Mei 2011, ikipendekeza wamiliki wa viwanja nchini, ukiwamo wa Benjamin Mkapa, kuboresha viwanja vyao na kuweka vifaa vya kisasa kuwezesha wapenzi wa soka kukaa uwanjani kwa raha bila bugudha, huku wakipata huduma za chakula na vinywaji.

# MEHATA yapongeza serikali kutenga fedha kwa afya akili

**Na Christina Mwakangale**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili (MEHATA), Dk. Said Kuganda, ameipongeza serikali kwa mara ya kwanza kutenga Sh. bilioni 9.1 kwa ajili ya afya ya akili.

Pia amepongeza kuanzishwa mtaala wa Stashahada ya Juu ya Afya ya Akili kwa Wauguzi, ambayo itaanza kudahili wanafunzi wa mwaka wa masomo 2024/25.

Dk. Kuganda ambaye ni Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na Nipashe.

Alisema fedha hizo zitaimarisha huduma ya afya, elimu, kuongeza wataalamu na matibabu kwa wenye matatizo ya akili, akiutaja unyanyapaa bado ni kikwazo katika kuongeza idadi ya kuwafikia wanaougua.

"Napongeza serikali kwa mara ya kwanza kuelekeza kabisa fedha kwa ajili ya eneo hili. Awali, fungu la afya ya akili lilijumlishwa na magonjwa yasiyoambukiza (NCD). Bajeti hii itaongeza wigo wa huduma kwa wanaougua na kutoa elimu kwa umma.

Bingwa huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi wa Watoto wenye Kifafa Tanzania (UWAKITA), alisema bado kuna elimu duni kuhusu magonjwa ya akili na wanaougua kifafa, jamii ikidhani ni ugonjwa mmoja, hivyo elimu inahitajika.

"Kwenye changamoto watu wanachanganya anayeugua kifafa, ndiye mwenye magonjwa ya akili, lakini wagonjwa wa kifafa sio wagonjwa wa akili.

"Wagonjwa wa kifafa wanavyowapa majina, wanavyotengwa inaweza kuwafanya wakaingia katika kundi la wenye matatizo ya akili, kutokana na kuathiriwa na dhana, tafsiri zisizo na ukweli," alisema.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo juzi, bungeni mkoani Dodoma, alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, zimetengwa Sh. 9,318,528,988 kwa ajili ya afya ya akili.

Alisema katika vipaumbele 10 vya wizara kwenye bajeti hiyo, kiko mahususi kwa ajili ya afya ya akili, lengo likiwa kuimarisha huduma za utengamao kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

# Nchi nne zafungua ofisi ndogo ubalozi Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imesema hadi sasa nchi nne zimeshafungua ofisi ndogo za ubalozi jijini Dodoma.

Nchi hizo ni Ufaransa, Ujerumani, China na Uingereza pamoja na Ofisi ya Uratibu ya Umoja wa Mataifa (UN).

Naibu Waziri, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (pichani), aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini Balozi mbalimbali zitahamia Dodoma kuunga mkono juhudi za serikali kuhamia Dodoma.

Akijibu swali hilo, Balozi Mbarouk alisema wizara inaendelea kuzishawishi nchi zingine kufungua ofisi zao Dodoma.

"Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuzishawishi balozi zote zinazowakilisha nchi zao hapa nchini kuhamia makao makuu ya nchi Dodoma. Tayari serikali imetenga eneo maalum la kujenga ofisi za kibalozi na makazi ya mabalozi na tayari hati za viwanja hivyo zimeanza kutolewa," alisema.

Alisema serikali inaendelea pia kuzihamasisha balozi kwa kuwafahamisha juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali za kuboresha miundombinu katika jiji la Dodoma ambayo ni muhimu kwa mabalozi hao katika utekelezaji wa majukumu yao pindi watakapohamia.



"Kutokana na juhudi hizo ziko balozi kadhaa ambazo zimeishaleta wataalamu wake ili kukagua viwanja hivyo na sasa wanaandaa michoro ya majengo watakayojenga," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Chombo kudhibiti gharama huduma za afya ni muhimu

**WAKATI** Waziri wa Afya akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya bajeti ya wizara yake juzi bungeni, alisema serikali inakusudia kuja na chombo muhimu kitakachokuwa kinadhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi.

Afya ni muhimu sana katika maisha ya binadamu hivyo ni lazima suala la gharama liangaliwe ili lisiwaumize wananchi.

Chombo hicho tumeelezwa kuwa kitakuwa kinafanyakazi ya kusimamia kama ilivyo kwenye gharama za ulipaji maji, umeme na mafuta.

Na kwamba lengo ni kudhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi hususan wasio na bima ya afya.

Utaratibu huu utasaidia kudhibiti ule utozaji wa gharama holela unaofanywa na baadhi ya madaktari katika hospitali za binafsi na zile za serikali ili kuwapa unafuu wananchi.

Vyombo kama hivi vimefanikiwa pia katika huduma za mafuta ya petroli ambapo inafahamika kila mtu anapokwenda kwenye kituo cha mafuta kujaza kwenye gari yake anakuta bei elekezi.

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa wanapokwenda kutibiwa kukuta wakitozwa gharama kubwa kumuona daktari kabla ya kupata matibabu, hali inayowafanya wasiokuwa na bima za afya kushindwa kulipia na kuamua kwenda kujaribu tiba zingine mbadala.

Kwa mujibu wa wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Fedha, kwenye vitita vya NHIF, madaktari bingwa katika ngazi ya rufani mkoa, ada imeongezeka kutoka Sh. 15,000 hadi 25,000 ambayo ni sawa na kumuona daktari aliyepo ngazi ya kanda na taifa.

Kiwango hichi cha kumuona daktari kinatoa hamasa kwa madaktari hao kufanyakazi katika mazingira yoyote watakayopangiwa, ikiwamo pembezoni.

Aidha, ada ya usajili na kumuona daktari kwa wanufaika wa NHIF kwa ngazi ya wilaya imeongezeka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 7,000 kwa ngazi ya zahanati ada imeongezeka kutoka Sh. 1,000 mpaka Sh. 3,000.

Aidha, kitita hicho kitaboresha upatikanaji wa huduma bora za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchama.

Aidha, kitita hicho kimezingatia maendeleo ya teknolojia ya tiba, hali halisi ya bei katika soko na uwezo wa mfuko kugharamia huduma hizo huku ukiendelea kuwa endelevu kwa kuzingatia ushauri wa taifa, mapendekezo ya tathmini ya uhai na uendelevu.


Wizara ya Afya pia imetaja vipaumbele na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.

Katika bajeti hiyo wizara imetenga Sh. bilioni 117.61 kuimarisha huduma ya kinga dhidi ya magonjwa ikiwamo kuimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa kuwafikia watoto 3,117,564 wenye umri chini ya miaka miwili, wasichana 871,429 wenye umri wa miaka tisa na wajawazito 3,298,437.

Kwa mujibu wa waziri, Sh. bilioni 17.18 zimetengwa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, ikiwamo kujenga, kukarabati na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa waliozaliwa na uzito upungufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mwandishi Wetu

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mama anzia jikoni kutumia nishati safi

**NI** dhahiri wengi wanakumbuka visa na mikasa ya kuwa na macho mekundu, ambayo yalisababisha vifo vya mamia ya wanawake wazee kwa kisingizio kuwa ni wachawi.

Hilo ni jambo lililoacha hatia kwa kumwaga damu na kukatisha maisha ya wanawake kwa ukatili wakikatwa mapanga na hata kuchinjwa, kwa vile moshi uliumiza macho yao wakahusishwa na uchawi.

Upikaji kwa kutumia nishati ni eneo ambalo limekuwa mwiba kwa taifa hili, hata vifo kwa wanawake. Ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuzichunguza na kuziboresha sekta zote, ameitazama afya ya mpishi jikoni.

Ni afya ya mama ambaye kwa Tanzania inayokadiriwa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), kuwa ina kaya takribani milioni 13.9, ndiye mpishi mkuu.

Sasa serikali inataka mama anayeandaa chakula awe timamu kwa kuhakikisha taifa linatumia nishati safi jikoni.

Hiyo ni kampeni ya Rais Samia, anayebeba ajenda ya nishati safi ya kupikia, akitaka kupunguzwa matumizi ya mkaa na kuni, mafuta ya taa na vinyesi vya wanyama jikoni ili kuwa na afya njema.

Kampeni hiyo ni usalama wa watu -afya na mazingira, hivyo, ni vyema tumpe Mama Samia maua yake kwa hatua anazochukua kwenye jambo hilo.

Niirejee tena simulizi au gumzo la miaka 1980 hadi 2010 iliyobeba taarifa za vifo vya wanawake wazee waliouawa mikoa ya kanda ya ziwa, yakiwa matokeo ya kutumia nishati chafu jikoni.

Mamia ya wazee hao waliokuwa wakipikia samadi ya ng'ombe huko Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kigoma na hata Rukwa walituhumiwa kuwa wachawi kisa walikuwa na macho mekundu.

Macho mekundu ni matokeo ya kupikia nishati chafu ya samadi ya ng'ombe na punda, yote yalisababisha wakati mgumu na mauti kwa wanawake.

Lakini, si hayo tu wapo ambao hawakuuawa kwa mapanga kwa kuitwa wachawi lakini walipata saratani za mfumo wa hewa na maradhi mengine yatokanayo na sumu na kemikali za nishati chafu.

Rais ameyatafakari hayo na mengine mengi na analeta ufumbuzi. Ameuona uhaba na ughali wa kuni na mkaa, vifo, uharibifu wa mazingira hasa misitu, kuzidi majanga ya asili ukame na mafuriko kuwa ni mambo yanayoambatana na nishati chafu ya kupikia.

Yanaambatana kwa sababu kuni na mkaa humaliza misitu, kupikia kinyesi na mafuta ya taa huongeza joto na hewa ukaa vyote vikichochea mabadiliko ya tabia nchi.

Mama wa Taifa, ameliona hilo na anahimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa maendeleo ya nchi na afya bora kwa wapishi ambao wengi ni wanawake.

Ikumbukwe kuwa nishati chafu inaongeza matatizo kwa sababu hakuna nyumba ambayo watu watalala bila kula, hivyo ni mzigo kwa mama kila wakati.

Lakini hivi sasa serikali imepiga stop ni lazima kubadilika kuanzia nyumbani, shuleni, hospitalini, majeshini, hoteli kubwa na za kisasa, nishati lazima iwe safi itumike gesi, umeme, bayogasi, kuni na mkaa mbadala.

Ni bashasha kutoka kwa kinamama wanaofurahia kuboreshwa huduma za jikoni kwa maana wengi wao ndiyo wapishi wa kaya takribani milioni 14 za taifa hili.

Hivyo kuanzia Arusha hadi Zanzibar kinamama wanampongeza Rais kwa kuwafikishia huduma hiyo inayojali na kulinda afya zao, mazingira na kuandaa taifa lilillo timamu.

Ni imani ya Watanzania kuwa amewaokoa na ataendelea kunusuru wengi lakini hasa wakinamama pamoja na watoto wao wadogo kwa wakubwa ambao wanatumia muda mwingi jikoni.

Wengi katika maeneo mbalimbali wamesikia, kuona au kuhakikisha kuwa serikali inakabiliana na changamoto ya nishati chafu inayotumika jikoni na sasa inaikomesha, hivyo waunge mkono.

Tukiachana na eneo la nishati chafu, ni kweli kuwa sehemu nyingi mijini na vijiji zilikuwa na shida kuanzia usafiri, vituo vya afya, elimu, maji na umeme, lakini serikali inaendelea kuondoa shida hizo hatua kwa hatua.

Pamoja na kumtua mama ndoo kichwani, kumpa huduma bora za afya na sasa kumpatia nishati safi ya kupikia, yote yatafanikiwa, iwapo Watanzania wataunga mkono na kushiriki kikamilifu kwenye juhudi hizo zinazolenga kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

HABARI KITAIFA

# Hatifungani ya Jamii yauzwa Soko la London

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetanua wigo wa kushiriki katika masoko ya mitaji kimataifa kwa kuorodhesha hatifungani yake ya jamii (NMB Jamii Bond) juzi katika Soko la Hisa la London (LSE).

Hatua hiyo inaifanya NMB kuwa taasisi ya kwanza Tanzania kuwa na hatifungani katika soko hilo kubwa kuliko yote ya hisa duniani na benki ya kwanza Afrika Mashariki, Kati na Kusini kuorodhesha hatifungani ya uendelevu LSE.

Kuorodheshwa kwa mara ya pili kwa NMB Jamii Bond katika masoko ya hisa ya nje kunafuatia kuidhinishwa kwake mwezi jana kuuzwa katika Soko la Hisa la Luxembourg ambako pia hatifungani ya NMB Jasiri Gender Bond imekuwa inafanya vizuri tangu iorodheshwe kwenye soko hilo mwaka jana.

Uzinduzi wa mauzo ya Hatifungani ya Jamii ulifanyika wakati wa ufunguzi wa shughuli za wiki hii za LSE, maarufu duniani kwa kuendeleza uwekezaji unaozingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, ufadhili wa uendelevu na uwekezaji wa kijani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Julia Hoggett, alisema LSE inajivunia kuhusishwa na dhamana hiyo anzilishi ya ufadhili wa uendelevu ya NMB ambayo ni ubunifu mahusus kwa ajili ya kuchochea uwekezaji katika miradi yenye tija kijamii na kimazingira.

Alisema hatifungani hiyo kubwa ya uendelevu kuwahi kutolewa katika ukanda huu pia ni fursa kwa wawekezaji kutengeneza faida huku wakichangia kuboresha maisha na kusaidia kuilinda asili ya dunia.

Benki ya NMB iliiweka sokoni NMB Jamii Bond mwaka jana na kupata Sh. bilioni 75 za Dola za Marekani milioni 10 kukiwapo fursa ya kuongeza Sh. bilioni 25 na Dola milioni tano.

Ikithibitisha ukopeshekaji wa benki hiyo na kuonesha utayari wa wawekezaji kuunga mkono ajenda ya uendelevu ya taasisi hiyo, mauzo ya Hatifungani ya Jamii yalizidi kwa asilimia 284 upande wa Shilingi na asilimia 730 kwa upande wa Dola na kupelekea kupatikana jumla ya Sh. bilioni 400 (Dola milioni 160).

Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna aliyeongoza maofisa wa NMB kushuhudia tukio hilo, alisema uorodheshwaji huo wa kihistoria unaiweka pazuri benki hiyo katika masoko ya fedha duniani na kwenye macho ya jumuiya ya wawekezaji wa kimataifa.

## Maofisa Polisi wapewa elimu mafao kidigiti

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) wametoa mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa na askari wa jeshi hilo kushughulikia mafao yao kidigiti.

Kamishna wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu wa jeshi hilo, CP Suzan Kaganda, akifungua mafunzo hayo juzi kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, alisema yametolewa kwa maofisa wanadhimu makao makuu, mikoa na vikosi pamoja na wasimamizi na watendaji wa dawati la mafao ndani ya jeshi hilo.

Alisema mafunzo hayo ya siku mbili yamelenga kutoa elimu ya namna ya uwasilishaji nyaraka za mafao kupitia mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kiongozi huyo wa jeshi aliwataka washiriki kusikiliza mada zote husan inayohusu mfumo mpya wa uwasilishaji nyaraka za maombi ya mafao mbalimbali ya watumishi katika mfuko huo (PSSSF).

Alisema mfumo huo unatoa urahisi kwa mwanachama kufuatilia kujua kila hatua ya madai ya mafao kwa kupitia simu janja.

Ni mfumo alioutaja unasaidia kuondoa kupotea kwa nyaraka za mafao wakati wa usafirishwaji na kujua eneo lenye mkwamo katika uwajibikaji wa kushughulikia ulipaji malipo ya mafao mbalimbali ya watumishi.

Akawataka watendaji wa Jeshi la Polisi kujikita katika matumizi ya TEHAMA, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyotoa katika mkutano wa maofisa wakuu waandamizi wa polisi uliofanyika Septemba 4, 2023 huko Oysterbay, Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-razaq Badru, alisema wanaendelea kuboresha huduma za mfuko, ikiwa ni pamoja na maboresho ya kupunguza udanganyifu.

"Tumeanzisha huduma mbalimbali, mojawapo ni PSSSF Kiganjani ili kuondoa usumbufu wa kupata taarifa za michango ya kila mwezi kwa wanachama wetu, zoezi linalokwenda sambamba na kutoa elimu kwa wanachama na wadau wote wa PSSSF," alisema.

Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akunai, alipongeza Jeshi la Polisi kwa kuratibu na kusimamia mafunzo hayo yenye lengo la kuboresha ufanisi na huduma kwa watumishi wa Jeshi la Polisi.


NMB Karibu yako

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 24 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB**

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 24 wa mwaka wa wanahisa wa Benki ya NMB utafanyika kwa njia ya mtandao siku ya Ijumaa tarehe 7 Juni, 2024 kuanzia saa 4 asubuhi. Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

24.1 MATANGAZO NA AKIDI
24.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
24.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 23 ULIOFANYIKA TAREHE 2 JUNI 2023
24.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 23 WA WANAHISA
24.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2023
24.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2023
24.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA VIWANGO VYA MALIPO YA WAKURUGENZI
24.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI
24.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2024
24.10 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria Mkutano lazima wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au Taarifa ya Akaunti (CSDR Account Statement).
2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya Benki ya NMB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe Mwantumu.Salim@nmbbank.co.tz kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Alhamis tarehe 6 Juni 2024.
3. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria kikao watahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya Benki ya NMB (www.nmbbank.co.tz).
4. Wakurugenzi wamependekeza malipo ya gawio la shilingi 361.18 kwa kila hisa, ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 180.59 kutokana na faida ya mwaka 2023.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **- 15 Mei 2024** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **- 15 Mei 2024** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **- 05 Juni 2024** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **- 06 Juni 2024 na kuendelea** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **- 10 Juni 2024** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa:** | **- 19 Juni 2024** |

**Kwa agizo la Bodi.**

Mwantumu Salim
**Katibu wa Kampuni**
15 Mei 2024

www.nmbbank.co.tz

NMB FOUNDATION

# Join Our Team as a Board Member

**Introduction to NMB Foundation:**

NMB Foundation is a not-for-profit Corporate Social Investment arm of NMB Bank Plc, which was established in 2021 to scale up its intervention in carefully chosen pillars that impact the lives of majority of Tanzanians. NMB Foundation programs are designed to address issues of relevance specifically within the thematic areas of Education, Health, Agriculture, Environment and Entrepreneurship. NMB Foundation dedicated to driving positive social change and sustainable development within our communities. With a keen focus on these five thematic areas, we have been actively working to create lasting impacts and meaningful transformation in the communities we serve.

**Objective:**

We are seeking experienced and dedicated individuals to join our Board of Directors. As part of our strategic growth, we aim to onboard two board members who share our passion for making a difference and possess the expertise to guide our organization forward.

**Qualifications and Criteria:**

1. Demonstrated commitment to the mission and values of NMB Foundation.
2. Expertise in areas relevant to our focus, such as agriculture development, economic empowerment, education, healthcare, and environmental sustainability.
3. Experience in board leadership, strategy development, and governance of NGOs.
4. Strong communication, networking, and interpersonal skills.
5. A track record of ethical leadership and decision-making.

**Main Responsibilities:**
**Governance and Strategic Leadership:**

- Provide visionary leadership and guidance to ensure NMB Foundation fulfills its mission and strategic objectives.
- Participate actively in the development and review of the Foundation's strategic plans and policies.

**Oversight and Accountability:**

- Setting strategic direction and approving major initiatives to ensure alignment with the foundation's mission and goals.
- Holding management accountable for financial management and performance through regular audits and financial reviews, ensuring transparency and trust among stakeholders.

**Fundraising and Resource Mobilization:**

- Advice and play an active role in fundraising efforts, contributing networks, connections, and personal philanthropy to support the Foundation's initiatives.
- Advice in identifying potential donors, sponsors, and partners for the Foundation's projects and programs.

**Program and Initiative Support:**

- Provide expertise, insights, and advice to guide the development, implementation, and evaluation of the Foundation's projects and initiatives.
- Support the Foundation's focus areas, such as economic empowerment, education, healthcare, environmental sustainability, and agriculture development.

**Advocacy and Networking:**

- Act as ambassadors for the Foundation, promoting its mission, values, and impact among stakeholders.
- Leverage personal and professional networks to create strategic partnerships and collaborations.

**Program and Initiative Support:**

- Provide expertise, insights, and advice to guide the development, implementation, and evaluation of the Foundation's projects and initiatives.
- Support the Foundation's focus areas, such as economic empowerment, education, healthcare, environmental sustainability, and agriculture development.

**Board Meetings and Participation:**

- Attend and actively contribute to board meetings, ensuring regular attendance and meaningful engagement.
- Prepare for meetings by reviewing materials, reports, and relevant documentation.

**Time Commitment:**

Dedicate time and effort to fulfill board responsibilities, including attending meetings, participating in committee work, and engaging in Foundation activities.

**Confidentiality:**

- Maintain strict confidentiality of sensitive information related to the Foundation's operations, beneficiaries, and stakeholders.

**Termination of Service:**

- Board members may resign from their position by providing written notice to the Board Chairperson.
- In exceptional circumstances, the Board may terminate a member's service due to non-compliance with board responsibilities, conflicts of interest, or other significant issues

**Selection Process:**

Interested candidates are invited to submit their CVs and cover letters via email to **nmbfoundation2024@nmbbank.co.tz** outlining their relevant experience and motivation to serve on the Board of Directors by **29th May 2024.** Shortlisted candidates will be invited for assessment of their alignment with the Foundation's values and objectives. If you encounter any challenges during the application process, please feel free to contact us at **0222322009/022232008.**

**Term of Appointment:**
Board members will serve an initial term of THREE years, with the possibility of renewal based on performance and organizational needs.

**Remuneration:**
The position of Board member is voluntary and non-remunerated. However, reasonable expenses incurred may be reimbursed.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

# HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2024/25



Mh. Abdallah Ulega (Mb)
Waziri Mifugo na Uvuvi



Mh. Alexander Mnyeti (Mb)
Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi



Prof. Daniel Mushi,
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)



Prof. Riziki Shemdoe,
Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi



Dkt. Edwin Mhede - Naibu Katibu Mkuu (Sekta ya Uvuvi)

# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

## MAENEO YA VIPAUMBELE SEKTA YA UVUVI KWA MWAKA 2024/2025

- Kununua Meli 1 ya Mafunzo ya Uvuvi
- Kununua Boti za Uvuvi 450
- Kuweka mazingira rafiki kwa wavuvi ili kuruhusu ongezeko la rasilimali kwenye maji ya asili
- Uanzishaji wa chombo cha kusimamia rasilimali za uvuvi,ukuzaji viumbe maj
- Kuongeza masoko ya mazao ya Uvuvi

# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

## MAENEO YA VIPAUMBELE SEKTA YA MIFUGO KWA MWAKA 2024/2025

- Kuongeza Uwekezaji kwenye sekta ya Mifugo
- Kuongeza Uzalishaji wa mazao ya Mifugo
- Kuongeza Vituo 8 vya BBT na kuimarisha vingine 16
- Kuchochea Ufugaji wa kisasa
- Kuongeza thamani na masoko ya mazao ya Mifugo

# HOTUBA YA MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB.) WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2024/2025

**A. UTANGULIZI**

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi); Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya mwaka 2024/2025 kwa Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb.), kuwa Naibu Waziri, na Dkt. Edwin Paul Mhede kuwa Naibu Katibu Mkuu –Uvuvi. Tunaamini ushirikiano wetu na mchango wa viongozi hawa vitaongeza kasi na kuleta mageuzi chanya, himilivu ya kisekta, ambayo ni mojawapo ya falsafa ya 4R za Mheshimiwa Rais kuelekea ujenzi wa uchumi jumuishi.

3. Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu, ninatoa pongezi kwa Viongozi Wakuu wa Serikali; akiwemo Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, kwa utendaji wao wa kazi uliotukuka unaomfanya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kuendelea kutoa mchango wake muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu na hivyo kung'ara katika duru za kitaifa na kimataifa.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo ni moja ya sababu zilizofanya uaminiwe na kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, ukiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Barani Afrika, na watatu Duniani kushika nafasi hiyo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia kwa umahiri mkubwa katika kuendesha shughuli za Bunge. Pia, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati zao katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

5. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb.), kwa kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Pia, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninawashukuru viongozi, wajumbe wote, na Sekretariati ya Kamati hii kwa kufanya uchambuzi makini wa Bajeti yetu. Ushauri wao umewezesha Wizara yangu kufanya maboresho stahiki. Tunaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya usimamizi na ushauri wa kuendeleza na kukuza mchango wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kwenye uchumi wa Taifa.

6. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb.) Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa Ushauri na ubunifu ulionisaidia kuboresha usimamizi wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, nawapongeza Prof. Riziki Silas Shemdoe (Katibu Mkuu-Wizara ya Mifugo na Uvuvi), Prof. Daniel Elius Mushi (Naibu Katibu Mkuu-Mifugo), Dkt. Edwin Paul Mhede (Naibu Katibu Mkuu-Uvuvi) na Bi. Agnes Kisaka Meena (Naibu Katibu Mkuu – Wizara ya Maji) aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Sekta ya Uvuvi) kabla ya uhamisho, kwa kuwa viongozi na watendaji wazuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Pia, nawashukuru kwa uongozi wao uliotukuka na kusimamia utendaji kazi wa Wizara. Vilevile, nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi hapa nchini.

7. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, naishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi Bi. Mariam Abdallah Ibrahim na watoto wangu, kwa kuendelea kuniombea na kunivumilia muda mwingi ninapokuwa kazini kutimiza majukumu yangu ya Kibunge na Kitaifa, na kwa kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu ya utumishi wangu kwa Watanzania. Aidha, nawashukuru kwa namna ya kipekee wananchi wote wa Jimbo la Mkuranga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuwatumikia na kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Naomba nichukue fursa hii kuwaahidi kwa nitaendelea kuwa mtumishi wenu na muda wote nitadumu katika kuwatumikia kwa umahiri na moyo wa dhati.

8. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na Watanzania wote, kwa kuondokewa na Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowasa, aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

9. Mheshimiwa Spika, natoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya, na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

10. Mheshimiwa Spika, pia, ninatoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyotokea maeneo ya Hanang', Rufiji, Kibiti, Kilwa, Kilosa, Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na maeneo mengine nchini ikiwemo, Mkuranga na Mafia yaliyopatwa na maafa. Ninawapa pole sana na kuwaombea ili Mwenyezi Mungu awape subra na kuwafanyia wepesi katika kuyajenga Maisha yao upya.

11. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024, kwa Fungu 99 na 64 na Mpango na Bajeti ya Fungu 99 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2024/2025, baada ya kuunganishwa kwa Fungu 99 na 64 kuwa Fungu moja 99. Hotuba hii inapatikana katika vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge na Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz. Aidha, naomba muhtasari huu pamoja na taarifa yangu niliyoiwasilisha iingizwe kwenye Hansadi zako

**B. SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99)**

**UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2023/2024**

**Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2023/2024**

12. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Wizara ilianza kutekeleza Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo ili kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa Pato la Taifa, na kupunguza umaskini. Maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa: Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo ili kuboresha mbari za mifugo; kuimarisha upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo; kuimarisha Afya ya Mifugo; kuboresha Huduma za Ugani; kuimarisha programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT); kuimarisha Huduma za Utafiti na Mafunzo ya Taaluma za Mifugo; kuwezesha uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake; kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO); na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli katika Sekta.

Fedha zilizoidhinishwa kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo 2023/2024

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 112.0. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 50.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha Shilingi bilioni 23.9 kwa ajili ya mishahara na Shilingi bilioni 26.2 matumizi ya mengineyo (OC). Aidha, Shilingi bilioni 61.9 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ikijumuisha Shilingi bilioni 56.6 fedha za ndani na Shilingi bilioni 5.3 fedha za nje. Hadi Aprili, 2024, jumla ya Shilingi bilioni 44.5 zimetolewa, sawa na asilimia 39.7.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida na Maendeleo**

14. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2024 Shilingi bilioni 32.1 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 64.1 ya Shilingi bilioni 50.1 zilizotengwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 18.63 zimetumika kulipa Mishahara na Shilingi bilioni 13.45 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

15. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024 Shilingi bilioni 12.44 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 20.1 ya Shilingi bilioni 61.9 zilizotengwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 12.40 ni fedha za ndani na Shilingi milioni 40 ni fedha za nje.

**Makusanyo ya Maduhuli**

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 99, ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 42.1. Hadi kufikia Aprili 2024, kiasi cha Shilingi bilioni 22.6 sawa na asilimia 53.68 zimekusanywa.

**Hali ya Sekta ya Mifugo**

17. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za mifugo na kuwezesha uzalishaji ambapo, idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka ng'ombe milioni 36.6 hadi ng'ombe milioni 37.9, mbuzi kutoka milioni 26.6 hadi milioni 27.6, na kondoo kutoka milioni 9.1 hadi milioni 9.4. Idadi ya kuku imeongezeka kutoka milioni 97.9 hadi milioni 103.1 ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 45.1 hadi milioni 47.4, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 52.9 hadi milioni 55.7 na nguruwe wameongezeka kutoka milioni 3.7 hadi milioni 3.9. Aidha, Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2023 ilikua kwa asilimia 5 na kuchangia asilimia 6.7 kwenye Pato la Taifa.

18. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2024, jumla ya ng'ombe 2,957,724 na mbuzi/kondoo 2,828,248 wenye thamani ya Shilingi trilioni 3.4, waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe 2,218,293 na mbuzi/kondoo 2,121,187, waliokuwa na thamani ya Shilingi trilioni 1.7 waliouzwa katika mwaka 2022/2023. Ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa minadani limetokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika soko la ndani na nje ya nchi pamoja na hamasa ya uvunaji wa mifugo.

19. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 803,264.3 mwaka 2022/2023, hadi tani 963,856.55 mwaka 2023/2024, ikiwa ni sawa na ongezeko la asimilia 16.7 (Kiambatisho Na. 2). Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 612,808.50; mbuzi tani 134,403.35; kondoo tani 28,290.00; kuku tani 132,442.28, na nguruwe tani 55,912.42 kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani 544,983.8; mbuzi tani 91,893.8; kondoo tani 21,888.05; kuku tani 96,915.6 na nguruwe tani 47,583.1 kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji katika kukinga mifugo dhidi ya magonjwa, wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi. Serikali inatoa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo lita 56,000 katika mikoa 25 na mashamba ya wizara na taasisi zake zenye thamani ya shilingi bilioni 2.5, ambayo imepunguza vifo vya mifugo kwa asilimia 8.

20. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya vipande 1,542,916 vya ngozi, vyenye uzito wa kilo 5,777,669.5 na thamani ya shilingi bilioni 7.0, viliuzwa nje ya nchi, ikilinganishwa na vipande vya ngozi 748,009, vyenye uzito wa kilo 3,591,396 na thamani ya shilingi bilioni 5.50, vilivyouzwa nje ya nchi mwaka 2022/2023. Aidha, mauzo ya ngozi kwenda nje ya nchi yameongezeka kutokana na mahitaji ya soko la ngozi isiyosindikwa kuongezeka katika nchi za Afrika Magharibi.

21. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, jumla ya vifaranga 95,584,347 vya kuku vimezalishwa na kusambazwa nchini ikilinganishwa na jumla ya vifaranga 83,845,967 vilivyozalishwa mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la asilimia 12.3. Kati ya vifaranga hivyo, vifaranga vya kuku wa nyama ni 73,481,572; chotara 14,163,396; na kuku wa mayai 7,939,379; ikilinganisha na vifaranga vya kuku wa nyama 64,457,555; chotara 12,424,064 na kuku wa mayai 6,964,348 kwa mwaka 2022/2023.

22. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho katika Mashamba ya Serikali umeongezeka kutoka tani 22.7, za mbegu za malisho aina ya nyasi na mikundekunde, mwaka 2022/2023, hadi tani 127.8 mwaka 2023/2024. Aidha, jumla ya marobota 267,695, ya hei yamevunwa katika mwaka 2023/2024, ikilinganishwa na marobota 248,209, yaliyovunwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na uwekezaji wa mashine na usambazaji wa zana na vifaa kwenye mashamba hayo. Pia, jumla ya tani 728.6 za saileji zimezalishwa. Vilevile, uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kufikia tani 1,880,000, mwaka 2023/2024, ukilinganisha na tani 1,580,000, mwaka 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na Serikali kuendelea kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi ili kuwezesha nchi kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya vyakula vya mifugo.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Sekta ya Mifugo**

**Sera, Sheria na Kanuni**

23. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ambapo rasimu ya kwanza iliyoboreshwa ipo katika hatua za maamuzi ya Serikali. Aidha, Wizara imekamilisha nyaraka za kuunganisha Bodi za Nyama na Maziwa na kupendekeza kuundwa kwa chombo maalum kitakacho simamia uendelezaji wa mazao na miundombinu ya Mifugo ambapo zipo kwenye hatua za mapitio katika ngazi za kiserikali. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeandaa Mpango Mkuu wa Mifugo, Uvuvi na Kilimo Mazao, (Agricultural Transformation Masterplan - 2050) ambao utatoa dira ya mabadiliko katika sekta hizo.

Uzalishaji Mbegu Bora na Masoko

24. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) imezalisha dozi 111,844 za mbegu za ng'ombe na kusambaza dozi 67,958, Aidha, Wizara imewajengea uwezo wahimilishaji 196 kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM).

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea na ujenzi na ukarabati wa minada 26 ya awali, upili na mpakani. Kati ya minada hiyo, minada saba (7) imekamilika. Aidha, minada 19 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kukamilika kwa ujenzi huu kutachangia kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo na kupunguza upotevu wa maduhuli kupitia utoroshaji wa mifugo.

**Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

26. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta 81,625.9 za maeneo ya malisho katika vijiji 194 vya Mikoa 16 nchini kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi na kufanya jumla ya maeneo yaliyotengwa kufikia hekta 3,466,111.43 kutoka hekta 3,384,485.5 mwaka 2022/2023.

**Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani**

**Huduma za Ugani wa Mifugo**

27. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imewezesha Mafunzo Rejea kwa Maafisa Ugani 1,058 katika Kanda Nane (8) ikihusisha mikoa 26 na halmashauri 184. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo





na Asasi zisizo za Kiserikali, imewapa mafunzo rejea jumla ya wafugaji 250,000 wakiwemo wafugaji wa mfano 620 kupitia mradi wa TIP3 unaotekelezwa na Heifer International Tanzania.

28. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta imeendelea: kusambaza teknolojia za ufugaji bora, kusindika mazao yatokanayo na mifugo, kuhifadhi malisho pamoja na kuwezesha upatikanaji wa masoko kupitia maonesho na maadhimisho mbalimbali. Aidha, jumla ya wadau 67,832 wamefikiwa kupitia maonesho ya Kimataifa ya Biashara – Saba Saba, maadhimisho ya wakulima - Nane Nane na Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani.

**Uratibu wa Utafiti na Mafunzo ya Mifugo**

29. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu, kuwezesha na kusimamia shughuli za utafiti wa mifugo nchini ambapo imefanya tathmini katika vituo saba (7) vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na uratibu wa Taasisi zingine 11 zinazofanya utafiti unaohusiana na Mifugo nchini. Lengo la tathmini hiyo likiwa kubaini tafiti mbalimbali zinazofanyika pamoja na uzingatiwaji wa sheria, kanuni, miongozo na utekelezaji wa agenda ya Utafiti wa Mifugo nchini ya mwaka 2020-2025. Aidha, tafiti hizi zimechangia katika utatuzi wa changamoto mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa mifugo ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa mbari za mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mifugo, upatikanaji wa mbegu bora za malisho na uboreshaji wa malisho ya asili.

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kufanya uratibu katika vyuo 21 vya mafunzo ya mifugo nchini ikihusisha tathmini ya mafunzo katika kampasi tisa (9) zilizo chini ya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA) na vyuo binafsi 12. Lengo likiwa ni kuona uzingatiwaji wa utumiaji wa mitaala ya wizara, uwiano wa wakufunzi na wanafunzi, na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

**Uchanjaji wa Mifugo**

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Serikali imeendelea kuratibu utoaji wa chanjo ya mifugo nchini ambapo hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya dozi 616,070,986 za chanjo ya mifugo zimetumika dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele kama ilivyobainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu ibara 66.

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengineo, Wizara ilipanga kujenga jumla ya majosho 246 yenye thamani ya Shilingi 5,658,000,000 katika halmashauri 65, fedha ambazo zilihamishiwa kwenye halmashauri ili kuwezesha ufanisi, tija na umiliki wa miradi hii kwa halmashauri husika. Aidha, uogeshaji wa mifugo unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya michovyo 1,342,932,142 ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe 660,725,421, mbuzi 453,142,239, kondoo 201,975,117 na punda 27,089,365.

Michovyo hii ni sawa na asilimia 75 ya lengo la michovyo bilioni 1.8 kwa mwaka 2023/2024.

**Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Mifugo**

**Kampuni ya Ranchi za Taifa**

33. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imezalisha ndama 1,361; kusambaza mitamba 201 kwa wafugaji ili kuboresha kosafu za mifugo; imezalisha na kuuza tani 186 za nyama; imenenepesha na kuchinja ng'ombe 1,534; imefyeka na kuondoa vichaka hekta 445 katika Ranchi za Kongwa, Ruvu na West Kilimanjaro kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho; imezalisha jumla ya robota 52,500 za malisho; imewezesha kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji 276 katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 505 kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini.

Bodi ya Nyama Tanzania

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeratibu mauzo ya nyama nje ya nchi, ambapo kiasi cha tani 13,745.38, zenye thamani ya dola za Marekani milioni 56.6 zimepatikana. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 12.3 ikilinganishwa na tani 12,243.8 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 51.9 zilizouzwa mwaka 2022/2023.

**Bodi ya Maziwa**

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Bodi ya Maziwa imesajili jumla ya wadau 411 wa maziwa. Idadi hii ni sawa na asilimia 103 ya wadau 400 waliolengwa. Pia, Bodi imefanya ukaguzi kwa wafanyabiashara 867 kati ya 1,200 waliolengwa sawa na asilimia 72.3 na hatua stahiki zilichukuliwa kwa wale waliokiuka sheria. Aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi iliyopelekea kuanza kwa uzalishaji wa maziwa ya unga hapa nchini itakayopelekea kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi. Maelezo ya kina yanapatikana katika ibara Na. 77 hadi 79 kwenye hotuba yangu.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA)**

36. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA) kupitia Taasisi ya kuzalisha chanjo (TVI) imezalisha na kusambaza chanjo za mifugo dozi 62,173,850 za magonjwa mbalimbali ya kipaumbele. Aidha, Wakala imefanya uchunguzi wa Magonjwa ya wanyama kwenye sampuli 21,667, kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo kwenye sampuli 2,550 na kutoa vibali 54 vya kuingiza viuatilifu vya mifugo nchini.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, TALIRI imeendelea kufanya tafiti za kuboresha mbari za mifugo na malisho ambapo jumla ya miradi 54 ya utafiti inaendelea kutekelezwa. Aidha, matokeo ya tafiti hizo ni kuibuliwa na kusambazwa kwa teknolojia, ambapo jumla ya mifugo iliyoboreshwa 268 ilizalishwa. Kati ya mifugo hiyo iliyozalishwa, 120 ilisambazwa katika mikoa ya Arusha, Dar-es-Salaam, Dodoma, Mbeya, Pwani, na Tanga. Aidha, TALIRI imewezesha upatikanaji wa ithibati ya mbegu za malisho aina tano (5) ambazo zitaanza kuuzwa katika maduka ya pembejeo.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

38. Mheshimiwa Spika, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) umedahili wanafunzi 4,454 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika kampasi nane (8) za Wakala ikilinganishwa na wanafunzi 4,036 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2022/2023. Idadi hiyo ni ongezeko la wanafunzi 418, sawa na asilimia 10. Aidha, Wakala umeendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau 600 katika Sekta ya Mifugo kuhusu mifugo na mazao yatokanayo na mifugo.

**C. SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64)**

**UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2023/2024**

**Maeneo ya Kipaumbele ya Sekta ya Uvuvi kwa Mwaka 2023/2024**

39. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi, imetekeleza maeneo saba (7) ya kipaumbele ambapo utekelezaji wake umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/2022 – 2025/2026), na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa: kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi, kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika Uchumi wa Buluu, kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu, kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji, kuimarisha uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na masoko; na kuimarisha huduma za ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

**Hali ya Sekta ya Uvuvi**

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa asilimia 1.9 na ilichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa. Aidha, Sekta inatoa ajira kwa watanzania zaidi ya milioni 6.0 pamoja na ajira ya moja kwa moja kwa wavuvi 198,475 na wakuzaji viumbe maji 35,986. Ajira hizi zimewezesha familia kupata kipato pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe ambapo Sekta huchangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama. Aidha, inakadiriwa kwamba kiwango cha ulaji wa samaki umefikia kilo 7.9 kwa mtu kwa mwaka.

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, hadi kufikia Aprili, Sekta ya Uvuvi imezalisha jumla ya tani 472,579.34 za mazao ya uvuvi. Kati ya hizo, tani 429,168.39 ni kutoka maji ya asili na tani 43,410.95 ni kutoka ukuzaji viumbe maji. Kufuatia uzalishaji huo, jumla ya tani 41,271.07 za mazao ya uvuvi na samaki hai 134,572 wa mapambo ziliuzwa nje ya nchi. Vilevile, Sekta inachangia katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na utalii ambapo hadi sasa kuna hifadhi tatu (3) za bahari na maeneo tengefu 15 yanayohifadhiwa kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU).

**D. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 – SEKTA YA UVUVI**

**Bajeti iliyoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 183.9. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 49.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 134.4 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2024, jumla ya Shilingi bilioni 103.2, sawa na asilimia 56.1 zimepokelewa.

**Matumizi ya Kawaida**

43. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2024, jumla ya Shilingi bilioni 21.9, sawa na asilimia 44.4 zimetolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi bilioni 11.2 ni fedha za mishahara ya watumishi (PE) na Shilingi bilioni 10.7 ni fedha za matumizi mengineyo (OC).

Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 134.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 110.7 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 23.7 ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2024, jumla ya Shilingi bilioni 81.2 sawa na asilimia 60.4 kutoka vyanzo vya ndani na nje zimetumika.

Makusanyo ya maduhuli

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi bilioni 41.0, kupitia Fungu 64. Hadi kufikia Aprili, 2024, Shilingi bilioni 24.7, sawa na asilimia 60.16, ya lengo la mwaka zilikusanywa kupitia Sekta ya Uvuvi. Hii ni sawa na asilimia 72.2 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni 34.2 hadi Aprili, 2024.

**Sera, Sheria na Kanuni**

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imekamilisha kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura Na. 388 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, Sura 280, ambayo yaliwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupitishwa na Kamati ya Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Kanuni za Ukuzaji Viumbe Maji ambayo imepitiwa na wadau mbalimbali na tayari rasimu hiyo imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki na kupata maoni. Pia, Wizara inaendelea na mapitio ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009.

47. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, Wizara imekamilisha nyaraka za kuanzisha chombo cha kusimamia shughuli za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ambacho kitakuwa na jukumu la kuendeleza, kusimamia, kudhibiti na kuhifadhi rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji nchini ambapo zipo kwenye hatua za mapitio katika ngazi za kiserikali.

**Uzalishaji wa Samaki Katika Maji ya Asili na Biashara ya Mazao ya Uvuvi**

48. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, jumla ya tani 472,579.34 za samaki, zenye thamani ya Shilingi trilioni 2.94, zilivunwa ikilinganishwa na tani 426,555.46 za samaki, zenye thamani ya Shilingi trilioni 2.86, zilizovunwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi (idadi ya wavuvi, aina na idadi ya vyombo vya uvuvi).

49. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea kuimarisha ukusanyaji, uchakataji na usimamizi wa taarifa na takwimu za uvuvi kwa lengo la kuratibu shughuli za usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Katika kipindi hicho wavuvi 198,475 na vyombo vya uvuvi 58,820 vilitumika katika shughuli za uvuvi ikilinganishwa na wavuvi 197,763 na vyombo vya uvuvi 58,448 kwa mwaka 2022/2023.

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha biashara ya mazao ya uvuvi katika soko la nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, jumla ya tani 41,271.07 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 134,572 wenye thamani ya Shilingi bilioni 515.78 waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrabaha wa Shilingi bilioni 14.44 ikilinganishwa na tani 29,466.98 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 150,308, wenye thamani ya Shilingi bilioni 453.80, waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrabaha wa Shilingi bilioni 12.56 katika mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 40.05 la mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi.

**Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi**

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo siku kazi 2,912 za doria, sawa na asilimia 37.3 ya lengo la mwaka la kufanya doria siku kazi 8,400, zilifanyika. Matokeo ya doria ilikuwa ni kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi na kuwachukulia hatua za kisheria waliotenda vitendo hivyo. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye ibara ya 106 hadi 115 ya kitabu cha hotuba yangu.

52. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilisaini Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Uvuvi katika Ziwa Tanganyika tarehe 16/12/2021 unaohusisha nchi nne (4) zinazozunguka ziwa ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Tanzania na Zambia. Mkataba huo, pamoja na masuala mengine, unahusisha kupumzisha shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa kipindi cha miezi mitatu (3) kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti kila mwaka. Lengo la kupumzisha ziwa ni kuruhusu samaki kuzaliana, kuimarisha kwa bioanuai na kuongeza uzalishaji wa samaki. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza Mkataba huo kwa kutoa elimu ikiwemo umuhimu wa upumzishaji wa ziwa pamoja na uanzishaji wa shughuli mbadala ambapo wadau wa uvuvi 6,898 walifikiwa. Pia, vizimba 29 vya kufugia samaki vimekopeshwa bila riba kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika kama shughuli mbadala wakati wa kupumzisha ziwa.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa samaki na bidhaa za uvuvi kwenye mipaka, maeneo ya viwanja vya ndege, na masoko ya samaki nchini kote. Aidha, kaguzi za kawaida 9,201 zilifanyika katika viwanda 21 vya kuchakata samaki; vituo 37 vya kuhifadhia samaki hai wa mapambo; mialo 33 ya kupokelea samaki; masoko matatu (3); maghala 70 ya kuhifadhia mazao yaliyokaushwa; vituo 17 vya kugandisha samaki; viwanda 17 vya mabondo; meli tatu (3) za uvuvi wa kambamiti na meli moja (1) ya uvuvi wa Bahari Kuu. Vilevile, ukaguzi ulifanyika katika vyombo 1,470 vya kusafirisha mazao ya uvuvi.

54. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekarabati miundombinu ikiwemo mitambo ya kuzalisha barafu na vichanja vya kuanika samaki ili kuongeza ubora na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Maelezo kwa kina yanapatikana Ibara 116 hadi 118 ya hotuba yangu.

Maabara ya Taifa ya Uvuvi

55. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Maabara ya Taifa ya Uvuvi ilipokea na kufanya uchunguzi wa jumla ya sampuli 1,982 za samaki, mazao ya uvuvi na mazingira. Maabara iliwezesha nchi kuuza tani 41,271.07 za samaki na mazao ya uvuvi katika masoko ya kimataifa, zenye thamani ya dola za Marekani milioni 206.6. Aidha, Maabara ilifanyiwa ukaguzi na Bodi ya ithibati ya SADC (SADC Accreditation Service - SADCAS) na kupewa ithibati ya ISO/IEC 17025:2017, na kuendelea kukidhi viwango vya ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi katika masoko ya kitaifa na kimataifa.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

56. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2024, uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji umefikia tani 43,410.95 kutoka tani 33,525.46 za mwaka 2022/2023. Uzalishaji huo unajumuisha tani 34,828.5 za samaki, tani 8,545.75 za mwani mkavu, tani 30 za kambakochi, tani 5.20 za kambamiti, tani 2.5 za kaa, tani 1.5 za majongoo bahari na vipande 250 vya lulu. Aidha, idadi ya miundombinu ya uzalishaji wa viumbe maji imeongezeka hadi kufikia mabwawa 34,417, vizimba 1,215 na vitotoleshi vya kuzalisha vifaranga 41 ikilinganishwa na mabwawa 32,878, vizimba 993 na vitotoleshi 39 mtawalia kwa mwaka 2022/2023.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, uzalishaji wa vifaranga vya samaki umefikia 66,684,806 ikilinganishwa na vifaranga 35,967,180 kwa mwaka 2022/2023 (Kiambatisho Na. 15). Aidha, matumizi ya chakula cha samaki nchini yameongezeka kutoka tani 4,337.9 mwaka 2022/2023 hadi tani 7,335.7 zinazojumuisha tani 3,309.9 zilizozalishwa nchini na tani 4,025.8 zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

58. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2024, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imetoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, uhifadhi na uongezaji thamani katika zao la mwani kwa wakulima 2,615.

59. Taasisi zilizo Chini ya Sekta ya Uvuvi

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania - TAFIRI**
**Utafiti Bahari ya Hindi**

60. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara

kupitia TAFIRI imefanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika maji ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu. Matokeo ya tafiti hizo katika baadhi ya maeneo ikiwemo Ziwa Tanganyika yameonesha kupungua kwa samaki. Matokeo haya, yamewezesha Wizara kuweka mikakati madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kufikia lengo la kuongeza wingi na uzalishaji wa samaki nchini. Maelezo ya kina yanapatikana katika ibara ya 131 katika hotuba yangu.

**Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi – FETA**

61. Mheshimiwa Spika, FETA imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 1,116 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada yanayotilia mkazo Umahiri kwa Vitendo na kuondokana na mfumo wa zamani wa Uwezo kwa Maarifa. Aidha, FETA imewezesha mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uelewa na kukuza ujuzi kwa washiriki 4,035 katika maeneo ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

62. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TAFICO, imesaini mkataba na Serikali ya Japan wa ujenzi wa meli moja (1) ya uvuvi wa bahari kuu ambapo uundaji wa meli umeanza mwezi Mei, 2024 na unategemewa kukamilika mwezi Disemba, 2025. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya majengo ya Shirika umefikia asilimia 75. Pia, TAFICO imenunua mtambo wa barafu za chenga wenye uwezo wa kuzalisha tani tano (5) kwa siku ili kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi. Vilevile, Shirika linaendelea na tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii kwa ajili ya ununuzi wa meli nne (4) za uvuvi wa Bahari Kuu na kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

63. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) ilifanya ukaguzi katika meli 75 za uvuvi, kati ya hizo meli 67 zilichukua leseni na meli nane (8) zilipewa vibali na ruhusa. Hivyo, kuwezesha makusanyo ya Shilingi bilioni 9.7 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 6.8 zilizokusanywa kutoka leseni 51 za mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2.9, sawa na asilimia 42.6. Aidha, Mamlaka imeendelea kutumia mifumo ya ufuatiliaji wa mienendo ya meli (VMS) na kuweka Waangalizi wa Uvuvi.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) iliendelea kutekeleza jukumu la ulinzi na usimamizi wa rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo mapya ya hifadhi za bahari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi. Aidha, doria 420 za kwenye maji na nchi kavu zilifanyika ili kudhibiti uharibifu wa mifumo ikolojia ya rasilimali muhimu za bahari.

Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Programu ya ASDP II

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa-Masoko unaotarajia kukamilika mwaka 2025, ambao hadi Aprili, 2024 ujenzi umefikia asilimia 53. Maelezo ya kina yanapatikana katika ibara ya 150 ya kitabu cha hotuba yangu

Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (Extended Credit Facility-ECF)

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Programu maalum ya kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Programu hiyo inatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kupitia dirisha la ECF. Aidha, kupitia programu hiyo boti za kisasa za uvuvi 160 na vifaa vyake zimekopeshwa bila riba kwa wanufaika 3,295. Pia, katika awamu ya kwanza vizimba 222 vya kufugia samaki na pembejeo zake vimetolewa kwa wanufaika 1,214. Mikopo hiyo inatolewa kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)

**Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora kwa Vijana na Wanawake (BBT)**

67. Mheshimiwa Spika, Wizara ilipokea maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu kuanzisha Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) inayolenga kuwajengea uwezo vijana na wanawake kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imeendelea na utekelezaji wa Programu hiyo.

68. Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo hayo, Sekta ya Mifugo, imeanzisha vituo nane (8) vya vijana na wanawake kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji kibiashara. Aidha, mafunzo yametolewa kwa wanufaika 235 ambapo, kati yao, 74 wamepata ajira Serikalini na 161 wanaendelea na mafunzo. Kupitia Programu hiyo, jumla ya ng'ombe 3,388 wamenenepeshwa na kuuzwa kwa thamani ya Shilingi bilioni 1.97 na kupata faida ya Shilingi milioni 199.57. Vilevile, vijana wanaendelea na utekelezaji wa Programu hiyo hadi Juni, 2024 ambapo watakuwa tayari kwenda kuanza ufugaji wa kibiashara kupitia vitalu vilivyoandaliwa na Wizara katika Ranchi za NARCO za Kitengule na Kagoma.

69. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha usimamizi na kuongeza umiliki, Wizara imehamishia jukumu la kusimamia na kuendesha vituo nane (8) vya BBT-Mifugo vilivyopangwa kutekelezwa mwaka 2023/24 kwa Sekretariati za Mikoa mitano (5) ya Tabora, Arusha, Morogoro, Pwani na Mtwara.

70. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Programu hiyo inalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa kuwapatia mafunzo kwa vitendo, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Jumla ya wanufaika 500 (vijana na wanawake) wamepatiwa mafunzo ambapo wanufaika 200 wamehitimu na 300 wanaendelea na mafunzo katika vituo 15 vilivyopo Ukanda wa Ziwa Victoria (10), Ukanda wa Pwani (4) na Zanzibar (1).

**Ushiriki wa Sekta Binafsi**

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeendelea kushirikiana na wadau wa Sekta Binafsi wakiwemo, wazalishaji, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wengine wa mazao ya mifugo na uvuvi. Kupitia ushirikiano huo, wadau wa mifugo na uvuvi wameunganishwa na taasisi za fedha. Hadi kufikia Aprili mwaka 2024, benki ya TADB Shilingi bilioni 15.82, benki ya NMB imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 67.9 na benki ya CRDB Shilingi bilioni 66.59. Mikopo hiyo ililelekezwa kwenye maeneo ya ufugaji wa ng'ombe, kuku, nguruwe na samaki; uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo, kilimo cha mwani; unenepeshaji wa mifugo na uchakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi.

**E. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025**

72. Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/2025, umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt.Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili 2021.

73. Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/2025, pia yamezingatia falsafa ya 4R ya Mheshimiwa Rais inayosisitiza uwepo wa maridhiano (Reconciliation) uhimilivu (Resilience), mageuzi (Reforms) na kujenga upya (Rebuilding) ili kujenga uchumi jumuishi. Aidha, kwa upande wa Maridhiano tumejielekeza kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kwa kuanzisha miradi ya uzalishaji wa malisho na kutenga ardhi ya maeneo ya malisho. Vilevile, ili kuleta Uhimilivu kiuchumi, Wizara itatekeleza miradi ya vizimba, kilimo cha mwani, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na programu ya BBT. Pia, katika kuleta Mageuzi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeanzisha Mpango Mkuu wa Mageuzi ya sekta za Mifugo, Uvuvi na Kilimo Mazao (Agricultural Transformation Masterplan - 2050) utaohusisha uwekezaji ikiwemo uvuvi wa Bahari Kuu. Katika Kujenga Upya, Wizara itaendelea kuimarisha hifadhi za bahari na maeneo tengefu ili kulinda mazalia ya samaki na kukuza utalii ikolojia. Aidha, Vipaumbele pamoja na miradi na shughuli zitakazotekelezwa na Wizara pamoja na taasisi zake ni kama ifuatavyo:

**Vipaumbele vya Mpango na Bajeti**

74. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025 maeneo ya kipaumbele ya Mpango na Bajeti ya Wizara yatakayotekelezwa ni:- Kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi; Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi; Kuhamasisha uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi; na Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika sekta za mifugo na uvuvi.

**Miradi na shughuli zitakazotekelezwa**

**Sekta ya Mifugo**

75. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi na shughuli zifuatazo:

(i) Kufanya kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo kwa kutoa chanjo kwa magonjwa 13 ya kipaumbele;
(ii) Kuendelea na taratibu za uundwaji wa chombo kitakachosimamia uendelezaji wa miundombinu na mazao ya Mifugo;
(iii) Kuanza kutekeleza Mradi wa Mageuzi katika Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (T-CSDTP) wa miaka mitano (5) utakao nufaisha walengwa 600,000. Mradi utahusisha kununua ng'ombe wa kisasa wa maziwa 17,200; kujenga mabanda ya kisasa 5,000 ya ng'ombe; kujenga mfumo wa uvunaji maji ya mvua katika kaya 22,400; kununua na kusanikisha mitambo 2,800 ya biogesi; kujenga vituo 950 vya kukusanya maziwa; kununua dozi 929,000 za chanjo za mifugo; na kujenga kilomita 140 za barabara katika maeneo ya mradi;
(iv) Kuanzisha Guest House ya Mifugo (Livestock Guest House) katika Ranchi ya Mkata;
(v) Kununua na kusambaza madume 60 ya mbari bora za mifugo aina ya Brahman ili kuongeza uzalishaji na tija katika mnyororo wa thamani wa mifugo na mazao yake;
(vi) Kujenga kituo cha mafunzo ya wadau wa mnyororo wa thamani wa malisho aina ya mabingobingo (Juncao);
(vii) Kuboresha na kuendeleza hekta 20,000 za maeneo ya malisho katika eneo la Msomera, Kitwai na Saunyi;
(viii) Kukamilisha ujenzi wa mabwawa saba (7) na visima virefu vitatu (3);
(ix) Kuziwezesha LITA na FETA kutekeleza Programu ya elimu na ujuzi wa kazi za uzalishaji (Education and Skills for Productive Jobs Program-for-Results - Phase II);
(x) Kuwezesha mradi wa Maziwa Faida TALIRI Tanga na African Dairy Genetic Gain katika Mikoa saba (7) nchini;
(xi) Kuwezesha biashara za kimataifa za mifugo na mazao yake kwa kuwekeza katika kituo cha karantini cha Kwala; na
(xii) Kuzalisha dozi milioni 90 za chanjo za mifugo kupitia Wakala ya maabara ya Veterinari (TVLA).

**Sekta ya Uvuvi**

76. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa nguzo muhimu za uzalishaji hapa nchini. Kwa sasa usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye bahari na maziwa hususan maji ya ndani (Inner Waters) na maji ya kitaifa (Territorial Waters) unategemea zaidi mbinu za doria na operesheni ambazo matokeo yake ni ya muda mfupi na vitendo viovu vya uvuvi haramu hujirudia. Vile vile, mbinu hizi zinasababisha changamoto mbalimbali ambazo waheshimiwa wabunge na wananchi wameendelea kuzipazia sauti.

77. Mheshimiwa Spika, tunakusudia tuandike historia ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais shupavu wa Awamu ya Sita kwa kumaliza kadhia ya uvuvi haramu kwa kuweka na kutekeleza mikakati madhubuti ya muda mfupi na mrefu. Mkakati mmojawapo ni kutumia teknolojia za kisasa ambazo pamoja na kudhibiti (control) zitazuia (deterrence) uhalifu wa uvuvi katika bahari na maziwa yetu. Teknolojia hizo ni kama vile matumizi ya ndege maalum zisizokuwa na rubani (drones) ambazo zina uwezo wa kusafiri kilomita 100 kwa muda wa saa mbili (2) na kuchukua picha za kiwango cha juu (high resolution videos) za uhalifu wa uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi. Teknolojia hii itaongeza ufanisi na kupunguza matumizi ya rasilimali fedha na muda.

78. Mheshimiwa Spika, Wizara pia, inakusudia kuanza kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa kielektroniki ambao utafungwa katika vyombo vyote vya uvuvi zikiwemo boti za kisasa zilizotolewa hivi karibuni. Mfumo huu utafuatilia mienendo yote ya wavuvi nchini ikiwemo kuweka kumbukumbu za mavuvi. Pamoja na kuzuia uvuvi haramu, mfumo huu utasaidia kuweka usalama wa wavuvi na wananchi ambao wanapata matatizo wakiwa maeneo ya maji yetu. Aidha, Wizara itaweka mipaka na kulinda mazalia na makuzi ya samaki (critical habitats) kwa kuweka maboya maalum, hatua hii itazuia uharibifu wa mazalia ya samaki ambayo ndio chanzo cha utunzaji wa demografia ya samaki ndani ya maji yetu.

79. Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwekeza katika teknolojia sahihi zitakazowezesha uendelevu wa rasilimali zetu adhimu za uvuvi kwa maslahi mapana ya sasa na vizazi vijavyo. Aidha, katika mwaka 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi na shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa – Masoko na kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Bagamoyo;
(ii) Kuendelea na taratibu za uundwaji wa chombo kitakachosimamia uendelezaji wa rasilimali za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji;
(iii) Kuendelea na taratibu za ununuzi wa Meli nne (4) za uvuvi wa Bahari Kuu kupitia TAFICO;
(iv) Kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi na kiwanda cha kuzalisha vyakula vya samaki kupitia TAFICO;
(v) Kuwezesha ununuzi wa boti 450 na zana za uvuvi kupitia dirisha la ECF na Mradi wa TASFAM;
(vi) Kuwezesha vikundi 300 vya vijana na wanawake kwa ajili ya kilimo cha mwani, ufugaji wa kaa na majongoo bahari;
(vii) Kununua meli moja (1) ya mafunzo ya uvuvi kwa ajili ya FETA kupitia mradi wa TASFAM;
(viii) Kununua ndege saba (7) zisizo na rubani (drones), maboya 60 ya kubainisha maeneo ya mazalia ya samaki, na kusanikisha mfumo wa ufuatiliaji wa vyombo vya uvuvi;
(ix) Kuwezesha ununuzi wa vizimba 497 kupitia ECF;
(x) Kuanzisha mashamba darasa 20 ya ukuzaji viumbe maji katika Halmashauri 20; na
(xi) Kuzalisha vifaranga vya samaki milioni 85.

**Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT)**

80. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara inaendelea utekelezaji wa Programu ya BBT kwa kufanya shughuli zifuatazo:

(i) Kuendelea kusogeza Programu ya BBT mikoani kwa kuanzisha vituo vipya vinane (8) na kuimarisha vituo 16 katika mikoa mbalimbali;
(ii) Kuanza kutekeleza mradi wa BBT TALIRI – Kongwa ambao utahusisha ufugaji kibiashara wa kunenepesha mbuzi/kondoo 120,000, kuanzisha kilimo cha umwagiliaji wa malisho hekta 2,000; na kujenga kiwanda cha kuchakata vyakula vya mifugo; na
(iii) Kuwezesha vijana kufuga kibiashara ikiwa ni pamoja na unenepeshaji wa mifugo, kilimo cha mwani, ufugaji samaki katika vizimba; na ufugaji wa majongoo bahari.

81. Mheshimiwa Spika, katika kuchagiza utekelezaji wa shughuli za mifugo na uvuvi, Wizara yangu itaendeles kushirikiana na wadau na Taasisi mbalimbali zikiwemo WB, IFAD, EU, ASPIRES, IUCN, Irish Aid, FAO, JICA, UNDP, Botnar Foundation, SAGCOT, TNC, WCS, ILRI, UNICEF na WWF, Heifer International na balozi za nchi mbalimbali zikiwemo, Uholanzi, Norway, China, Komoro, Qatar, Jordan, Kenya, UAE, Kuwait, Oman, Saudia Arabia, EU, Italia na Vietnam

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025**

82. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99, inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 69,105,000,000, kati ya fedha hizo, Shilingi 36,105,000,000 zitatokana na vyanzo vya mifugo na Shilingi 33,000,000,000 vyanzo vya uvuvi. Vyanzo vikuu vya makusanyao hayo vinapatikana katika para 170.

**F. HITIMISHO**

83. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2023/2024 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za Kitaifa na Kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini, bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

84. Mheshimiwa Spika, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mkuranga ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya Taifa letu, nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu na watumishi wa wizara kwa kuendelea kunitia moyo ili niweze kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi.

**E. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025**

85. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara inaomba kutumia jumla ya Shilingi 460,333,602,000 kati ya fedha hizo, Shilingi 97,215,432,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 363,118,170,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida: Shilingi 97,215,432,000
• Mishahara Shilingi 44,847,492,000
• Matumizi Mengineyo (OC) Shilingi 52,367,940,000
(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo: Shilingi 363,118,170,000
• Fedha za Ndani Shilingi 242,078,803,000
• Fedha za Nje, Shilingi 121,039,367,000

86. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

***87. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.***





## Nape atoa maagizo REA usambazaji umeme

**Na Peter Mkwavila,** aliyekuwa KITETO

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ameagiza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kufikisha umeme kwenye minara inayojengwa ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji ikiwamo kutumia majenereta.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi katika ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mnara wa mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara inayojengwa na kampuni za simu kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Alisema minara mingi inatumia jenereta, hivyo kuna umuhimu wa wakala huo kufikisha umeme ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Aidha, aliwataka wananchi kutunza mnara huo uliojengwa katika Kijiji cha Kinua wiilayani hapa ambao umegharimu Sh. milioni 350 na ni mmoja kati ya minara 758 inayojengwa katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo ni lazima ilindwe.

Kuhusu umuhimu wa miundombinu hiyo ya huduma za mawasiliano, Waziri Nape alieleza kuwa ina manufaa makubwa kwa wakazi wa vijijini kwani inawawezesha kuwasiliana kwa urahisi, kutumia huduma za kifedha, kupata huduma za afya na elimu.

Aidha, Waziri Nape alipongeza UCSAF kwa jitihada za kuhakikisha maeneo ambayo kampuni za simu hazikufanikiwa kupeleka minara kutokana na sababu za kibiashara yanafikiwa kwa kufadhili ujenzi wa minara.

Alisema kuwa katika minara 758 iliyopangwa kujengwa mwaka wa fedha unaoishia 2024, kampuni ya Airtel imeongoza kwa kukamilisha miradi mingi zaidi kuliko kampuni nyingine za simu.

# Waziri azindua bomu baridi la kufukuza wanyama waharibifu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, amezindua bomu baridi ambalo litatumika kwa ajili ya kufukuza wanyama waharibifu hususani tembo.

Akizindua juzi kwenye viwanja vya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makutupora Kikosi cha 834 jijini hapa, Dk. Tax alisema litakwenda kusaidia kuondoa kero iliyokuwapo kwa wananchi kwa muda mrefu ya wanyama kuvamia maeneo ya makazi pamoja na mashamba.

Alisema bomu hilo litatumika kwa ajili ya kufukuza wanyama wavamizi katika makazi ya watu hususani tembo ambao hivi karibuni wamekuwa wakifanya uhalifu ikiwamo mazao, kujeruhi watu na wakati mwingine kusababisha vifo.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alipongeza Shirika la Mzinga kwa kugundua bomu hilo ambalo litakwenda kudhibiti tembo kwenye makazi na mashamba ya wananchi.

Alisema mabomu yao yatakwenda kujibu kero mojawapo ambayo imekuwa ikiathiri sekta ya utalii nchini ya migongano baina ya wanyama na binadamu.

Alibainisha kuwa shida ya tembo kuvamia makazi na mashamba siyo ya Tanzania peke yake bali ni bara zima la Afrika, hivyo watakwenda kuweka haki miliki ya bomu hilo ili kulinda umiliki.

Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga, Brigedia Jenerali Seif Hamis, alisema utafiti wa bomu hilo wameufanya kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori (TAWIRI).

"Mzinga na TAWIRI tulifanya utafiti wa bomu baridi tofauti na lile ambalo tulikuwa tunalitumia hapo awali kwa kuwa tembo walianza kulizoea lakini hili tumeboresha kwa kuongeza mlipuko lakini linalipuka likiwa juu tofauti na lile la awali," alisema.

Alisema tangu wakamilishe ugunduzi wa bomu hilo hadi sasa wamepata mahitaji mengi kutoka taasisi pamoja na halmashauri mbalimbali nchini.

Alisema; "Hadi sasa tunayo mahitaji 56,000 kutoka TANAPA, TAWA pamoja na halmashauri nyingine ambazo zinahitaji mabomu haya kwa ajili ya wanyama wavamizi hususani tembo."



Meneja Mkaazi wa Heineken Tanzania, Obabiyi Fagade (kulia), akishiriki kuweka mazingira mazuri kwenye kisiki cha mti uliokatwa ili uweze kuchipua upya katika msitu uliopo Kijiji cha Mpamantwa, wilayani Bahi, mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki, wakati wa kampeni ya kuokoa miti iliyokatwa na wanakijiji ili kurudisha hali nzuri ya misitu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nyama ya mbuzi kinara mauzo nje ya nchi

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema nyama ya mbuzi inaongoza katika mauzo nje ya nchi na inachangia asilimia 70.1 ya mauzo yote.

Alibainisha hayo juzi kwenye makabidhiano ya Kituo Atamizi cha Vijana cha ufugaji mbuzi kibiashara kilichojengwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), kwa ufadhili wa Serikali ya Denmark kupitia Mfuko Binafsi wa Kusaidia Wakulima (PASS TRUST).

Alisema mauzo ya nyama nje ya nchi yameendelea kuongezeka hadi kufikia Aprili, 2024 tani 11,682.3 (zikiwamo tani 870.7 za nyama ya ng'ombe, tani 8,059.38 za nyama ya mbuzi, tani 2,715.5 za nyama ya kondoo, tani 27.5 za nyama ya kuku na tani 9.3 za nyama ya nguruwe) zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 50.3 zilikuwa zimeuzwa nje ya nchi.

Alisema nyama ya mbuzi imeendelea kuongoza katika mauzo hayo na kwamba serikali inaendelea na jitihada za makusudi ili kuboresha utendaji wa sekta hiyo, ikilenga kuvutia na kunufaika zaidi na masoko ya kimataifa.

Alibainisha kuwa kwa sasa kuna nchi 12 zinazonunua nyama kutoka Tanzania na mikakati ni kuweka miundombinu na sera rafiki zaidi ili kuboresha sekta hiyo.

Majaliwa alisema serikali imeamua kuongeza Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutoka Sh. bilioni 66 hadi Sh. bilioni 295.9 mwaka huu ili kusukuma mbele mabadiliko makubwa na maendeleo katika sekta hiyo.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara na wasindikaji wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi kushirikiana na kituo hicho, ili kupunguza tatizo la upatikanaji ya mifugo bora kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na mazao yake.

Majaliwa alisema: "Nazisihi taasisi za fedha zione fursa hii ili kukaa na wadau katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji na usindikaji wa nyama ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji, nitoe wito kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ina jukumu la kusimamia sekta ya mifugo, iendelee kuweka mazingira bora ya uwekezaji ili kuwezesha sekta binafsi kufanya uwekezaji wenye tija na faida".

## Maofisa, askari magereza 627 wavalishwa nishani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAOFISA na askari wa Jeshi la Magereza Kanda ya Kati 627 wamevalishwa nishani walizotunukiwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Akizungumza jana kwenye tukio hilo, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, (CGP) Mzee Nyamka, alisema idadi hiyo inayojumuisha makao makuu ya Jeshi la Magereza, Bohari Kuu ya Magereza Mkoa wa Dodoma, Singida, Tabora na Iringa.

Kamishna huyo alisema katika jeshi hilo, Rais Samia alitunuku nishani kwa maofisa na askari 2,263 ambazo zimegawanyika katika makundi manne ikiwa ni pamoja na nishani ya utumishi uliotukuka, utumishi wa muda mrefu na tabia njema.

"Jeshi la Magereza lina maofisa na askari takribani 15,000 utaona siyo wote waliotunukiwa ni wachache na hawa wamejipambanua kutokana na hao wengine kuwa na nidhamu, maadili mema na utendaji wa kupigiwa mfano," alisema.

Alisema kwa wale ambao hawajabahatika kutunukiwa itakuwa ni chachu ya kuwafanya wazidishe juhudi kwenye utendaji wao kwa kuzingatia nidhamu, sheria, kanuni na taratibu ili awamu ijayo Rais Samia atakapotunuku nishani na wao wawe miongoni mwao.





# Mfumo ukusanyaji kodi na tozo kwa pamoja mbioni kukamilika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema inaendelea na mchakato wa kuandaa mfumo mmoja wa ukusanyaji wa kodi na tozo mbalimbali kwa wafanyabiashara nchini, ili kuondoa kero ya taasisi tofauti za serikali kukusanya kodi.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji aliyasema hayo juzi jijini Mbeya kwenye mkutano wa majadiliano kati ya sekta ya umma na binafsi uliokuwa na lengo la kujadiliana namna ya kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara nchini.

Dk. Kijaji alisema kero hiyo imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu na wafanyabiashara pamoja na wadau mbalimbali kuwa ilikuwa ikichangia kuua biashara na kufukuza wajasiriamali.

"Kilio hiki tumeshakisikia na kama serikali tunaendelea na majadiliano ya kuanzisha mfumo mmoja wa kukusanya mapato, yatakusanywa kwenye kapu moja kisha kila taasisi itapata mgawo wake na hivyo kupunguza usumbufu," alisema Dk. Kijaji.

Aidha, alisema serikali za Tanzania na Marekani zimeanzisha chemba moja ya wafanyabiashara nchini Marekani kwa lengo la kurahisisha ushirikiano wa biashara na kupunguza mlolongo wa usafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

Hivyo, aliwataka Watanzania kuwa waaminifu kwenye biashara ili kuepuka kuharibu masoko ya kimataifa akidai kuwa fursa hiyo ya soko la Marekani ni muhimu kulindwa pamoja na masoko mengine ya kimataifa.

Alisema wizara inaendelea na mazungumzo na Shirika la Ndege la Uturuki kwa ajili ya kuanza usafirishaji wa maparachichi yanayozalishwa nchini kwenda Uturuki ambako kuna soko kubwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, alisema wizara hiyo imekuwa ikishirikiana na vyombo mbalimbali kufanya operesheni za kukamata bidhaa bandia zinazoingizwa nchini ili kulinda viwanda vya ndani na afya za wananchi.

Alisema hivi karibuni walifanya ukaguzi kwenye mikoa mbalimbali nchini na kuwakamata baadhi ya wafanyabiashara wakiuza simu feki na hivyo wakachukua hatua za kisheria ikiwamo kutaifisha bidhaa hizo na kuwasweka ndani wahusika.

Pia, aliagiza taasisi zinazohusika na usimamizi wa ubora wa bidhaa nchini kuendelea kuchukua hatua kwa wale wanaokiuka ili kukuza viwanda vya ndani na kulinda usalama wa wananchi.

"Hatuwezi kuacha watu wanaingiza bidhaa feki nchini, bidhaa hizo ni hatari kwa uchumi wetu na kwa maisha ya wananchi, kwa hiyo niwahakikishie kwamba tutaendelea kuchukua hatua maana usalama wa Watanzania upo mikononi mwetu," alisema Abdallah.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga alisema utitiri wa kodi umekuwa ukisababisha kutoelewana kati ya wafanyabiashara na taasisi za serikali.

Alisema baadhi ya taasisi zinazokusanya kodi na tozo zimekuwa zikifanya kazi bila kuwashirikisha watu wa sekta binafsi ili na wao watoe maoni yao hali ambayo inaendelea kusababisha migogoro.

Alisema moja kati ya taasisi ambazo zimekuwa zikiwakwamisha wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) ambazo zimekuwa zikiwatoza tozo kubwa.

Mwakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Victoria Michael, alisema baadhi ya halmashauri na mikoa nchini imekuwa ikianzisha tozo mbalimbali ambazo zinakinzana na mpango wa taifa wa kuboresha mazingira ya biashara.

Alisema lengo la mpango huo ni kutatua kero za kibiashara zinazowakumba wafanyabiashara lakini zinapoanzishwa tozo mpya kwenye halmashauri ni uzalishaji wa matatizo mapya kinyume na lengo.

Victoria ambaye ni mchambuzi wa sera alisema sekta binafsi kwa sasa inachangia asilimia 50 na sekta ya umma inachangia asilimia 50 kwenye majadiliano ya kuboresha mazingira ya biashara.

Ofisa Mtendaji wa TCCIA Mkoa wa Songwe, Elijah Simbeye, alishauri serikali kutatua kero za kodi ikiwamo kuondoa utitiri wa kodi kwa kuziweka kwenye kapu moja ili kuwaondolea usumbufu wafanyabiashara.



Mmoja wa madereva bodaboda wa Jiji la Mbeya ambaye hakutambulika jina lake akiwa amewabeba watoto watano kwenye pikipiki Mafiati jijini humo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Hati miliki za kimila 700 kutolewa vijiji viwili

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HATI miliki za kimila zaidi ya 700 zinatarajiwa kutolewa kwa wananchi wa vijiji vya Suma na Nditu vilivyopo katika Kata ya Suma Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, itakayosaidia kupunguza migogoro ya ardhi.

Hati hizo zitatolewa baada ya kazi ya upimaji kukamilika utakaofanywa na Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi ambapo mradi huo kwa Wilaya ya Rungwe unatekelezwa katika vijiji viwili pekee.

Ofisa Ardhi kutoka Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi, Boniface Magige alisema mpaka sasa katika Kijiji cha Nditu wameandaa hati miliki 473 na Kijiji cha Suma hati 266 kwa ajili ya kutolewa kwa wananchi.

Alisema utaratibu huo unakwenda sambamba na utoaji wa elimu kuhusu matumizi bora ya ardhi kwa wananchi wa maeneo hayo, ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kutumia ardhi kwa kuzingatia mpango wa matumizi iliyowekwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nditu, Austine Lupogo, aliishukuru serikali kwa hatua ya kupima na kuwamilikisha wananchi wake maeneo kisheria hatua ambayo itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwapo kijijini hapo.

Alisema awali wananchi wake hawakuelewa mpango huo wakidhani una lengo la kuchukua maeneo yao lakini baada ya Tume ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kutoa elimu wamepata uelewa na wamefurahia hatua hiyo.

Mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Nditu, Agnes Sikwese, alisema mpango huo una manufaa kwa sasa na kwa vizazi vya baadaye kwa kuwa wamepata hati miliki ambazo zinawapa uhalali wa kumiliki maeneo yao.

Aidha, alisema kupata hati miliki kutawasaidia kupata fursa mbalimbali ikiwamo mikopo, huku akishauri mpango huo kuwa endelevu kwa wananchi wa vijiji vingine ili waweze kunufaika kama wao walivyonufaika.

# Qatar yatoa tani 120 za tende wakimbizi Kigoma

**Na Faustine Feliciane**

UBALOZI wa Qatar nchini Tanzania umetoa msaada wa tani 120 za tende zenye virutubishi kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), ili zigawiwe kwa wakimbizi katika kambi za Nyarugusu na Nduta mkoani Kigoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kukabidhi msaada huo, Balozi wa Qatar nchini Tanzania, Fahad Rashid AI Mareki alisema msaada huo kwa WFP unasisitiza dhamira thabiti ya Qatar katika kuendeleza juhudi za kibinadamu.

Alisema pia uimarisha mipango ya kimataifa inayolenga kupunguza uhaba wa chakula katika maeneo ya migogoro yenye watu wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Balozi Mareki alisema mchango huo umeimarisha ushirikiano wa Qatar, WFP pamoja na Tanzania kama mdau muhimu katika juhudi za kibinadamu duniani, inayojitolea kutoa misaada ya hali ya juu kwa watu binafsi wanaokabiliana na majanga migogoro, au dharura.

Alisema msaada huo unalenga kusaidia zaidi ya wakimbizi 200,000 kutoka katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi wanaoishi kwenye kambi hizo mkoani Kigoma.

"Msaada huo unaenea kwa wakimbizi 22,000 walio katika mazingira hatarishi ya lishe kama vile wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na wagonjwa hospitalini, kama sehemu ya mpango wa lishe wa ziada wa WFP," alisema Balozi Mareki.

Mkurugenzi na mwakilishi mkaazi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson, alisema mchango huo unakuja wakati WFP inakabiliwa na upungufu wa ufadhili na kusababisha kupatikana asilimia 60 pekee ya chakula kinachohitajika kwa wakimbizi.

"Tunaishukuru Serikali ya Qatar kwa mchango wao ambao umekuja kwa wakati, utatoa msaada wa chakula unaohitajika kwa wakimbizi ambao wanategemea tu usaidizi wetu WFP," alisema Gibson.

Alisema msaada huo umekuwa wa kwanza kutolewa na nchi hiyo kwa wakimbizi waliopo Tanzania kupitia WFP na anatarajia ushirikiano huo utaendelea.

Sarah alisema WFP hutoa vikapu vya chakula kila mwezi vinavyojumuisha nafaka zilizoongezwa lishe, mboga na mafuta ya kula.

Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Dk.George Fasha alisema WFP imekuwa mshirika wa muda mrefu kati ya mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo yamekuwa yakitumia kikamilifu Bandari ya Dar es Salaam katika shughuli zake.





## 'Ukarabati jengo la Majestic kutatangaza utamaduni'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji wa Tume ya UNESCO ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Profesa Khamis Malebo amesema ukarabati wa jengo la Majestic sinema visiwani hapa kutasaidia kutangaza utamaduni wa nchi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua warsha ya kujadili matumizi mazuri na uzinduzi wa ukarabati wa jengo hilo la kihistoria visiwani hapa.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaliwezesha jengo hilo kuendelea kuonesha sinema mbalimbali ikiwemo ya "Royal Tour" na "Serengeti haitaangamia" pamoja na maonesho ya kiutamaduni, jambo ambalo litatoa fursa ya kuitangaza nchi kwa watalii watakaofika katika jengo hilo.

Alisema juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kila kitu katika jengo hilo kinabaki kuwa salama na kuendelea kutumika kama sehemu ya historia.

"jengo hili limebeba kumbukumbu za sinema mbalimbali za zamani ikiwemo mikanda na mashine zilizokuwa zikitumika kuoneshea sinema kwa wakati huo ambazo hazipatikani kokote, hivyo kuendelea kutumika kwa jengo hilo kutawasaidia vijana wasasa kuona maendelelo ya teknolojia ya filamu ilipotoka hadi sasa." alisema Malebo.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Hifadhi Mjimkongwe Zanzibar, Ali Said Bakar alisema mradi huo utasaidia kurejesha baadhi ya vitu vilivyopotea ikiwemo maonesho ya sinema.

Aidha, alisema kuwa ukarabati huo hautaathiri mwonekano wa jengo hilo na kuhakikisha linabakia katika hali yake ya asili na kuendelea kubakia kuwa jengo la kihistoria.

Alisema kuwa jengo hilo mbali ya kuwa kituo cha utamaduni lakini pia litatoa fursa kwa wajasiriamli kuuza biashara zao kwa wageni na wazawa pindi watakapofika kupata huduma maeneo hayo.

Pia, aliwataka wananchi na watumiaji wa Mjimkongwe kuwa wastahmilivu katika kipindi chote cha ukarabati wa jengo hilo, akisema lengo ni kuliimarisha na kuleta maslahi kwa jamii na taifa.

Sheha wa Mnazimmoja, Mohammed Juma Mugheir, aliitaka Serikali ya Zanzibar kuangalia majengo mengine ndani ya Mjimkongwe yenye uwezekano wa kuwapatia wasanii wa utamaduni kufanyia kazi zao.

# Zanzibar, Brazil zakubaliana ujenzi miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameihakikishia Serikali ya Brazil ushirikiano mzuri, hususani kwenye miradi ya maendeleo.

Aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipozungumza na balozi mpya wa Brazil nchini Tanzania, Gustavo Martins Nogueira aliyefika kujitambulisha.

Katika mazungumzo yao walizungumzia uhusiano uliopo baina ya Zanzibar na Brazil kwenye nyanja mbalimbali za miradi ya maendeleo ikiwamo sekta ya afya, miundombinu ya barabara, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Pia walizungumzia kuimarisha ushirikiano wa biashara, utalii pamoja na fursa za uwekezaji kwenye sekta ya mafuta na gesi Zanzibar.

Kuhusu sekta ya biashara, Dk. Mwinyi alimweleza balozi huyo kwamba Zanzibar haina eneo kubwa kwa kilimo badala yake imejikita zaidi kwenye sekta ya utalii na uchumi wa buluu.

Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanbar itadumisha ushirikiano wake na Brazili hususani kwenye biashara ya sukari na mchele ili kupungumza mfumuko wa bei za bidhaa hizo nchini.

Alisema, Zanzibar imejaaliwa visiwa vizuri vyenye mvuto vya Unguja na Pemba vyenye ardhi ya uwekezaji, hivyo alimweleza balozi huyo kuangalia fursa ya uwekezaji kwenye sekta ya mafuta na gesi ambako serikali imeelekeza nguvu kuvutia wawekezaji.

Akizungumzia sekta ya afya, Dk. Mwinyi alimweleza balozi huyo nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeleza ushirikiano mzuri uliopo baina yake na Brazili.

Pia alimweleza kuendelea kutoa ushirikiano kwa timu ya madaktari wa Brazil wanaokuja Zanzibar kwa nia ya kuendeleza ushirikiano kwenye sekta ya afya hasa kwa sekta ya afya ya uzazi.

Balozi Nogueira alisema ushirikiano wa pande hizo mbili za diplomasia na kwamba Serikali ya Brazil itaelekeza nguvu zaidi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa kwenye eneo la afya ya uzazi.

Kuhusu ushirikiano wa biashara, Nogueira pia alimweleza Dk. Mwinyi kwamba Brazili ni mzalishaji mkubwa wa sukari duniani, hivyo aliitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushirikiana zaidi kwenye eneo hilo.

Kuhusu sekta ya miundombinu ikiwemo ya barabara na mawasiliano, Balozi Nogueira alimwakikishia Dk. Mwinyi kuwa Brazil inaendeleza ushirikiano wake na Tanzania hususani Zanzibar kwa kuangalia uwekezaji na kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba.




Mkurugenzi Mkuu wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel (kushoto), akikabidhi nyaraka za taasisi hiyo, kwa Mkurugenzi wa Elimu ya Juu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Aida Maulidi Juma alipotembelea na ujumbe wake katika ofisi za Global, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ali Abdulgulam Hussein (wa pili kulia) na Meneja wa GEL Zanzibar, Zulfiya Zameer. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali kuendesha operesheni kamata wakala elimu 'feki'

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema itaendesha msako na kuzifutia usajili wakala wa elimu ya nje ambao wanafanya kazi kwa ubabaishaji.

Hayo yalisemwa jana visiwani hapa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, alipotembelea ofisi za Global Education Link (GEL).

Alisema wizara inatambua kazi nzuri zinazofanywa na baadhi ya wakala wa elimu lakini kuna taaasisi zimeingia kwenye fani hiyo na kufanya kazi kwa ubabaishaji hali ambayo imesababisha malalamiko mengi.

Alisema kuna vijana nchini wakiwamo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakirubuniwa na baadhi ya mawakala wa mfukoni wasio waaminifu, hali ambayo imesababisha malalamiko mengi.

Alisema: "Mollel tuletee taarifa rasmi kuhusu wazo lako nitaelekeza ofisi yangu iratibu suala hili na kutushauri kwa sababu Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Mwinyi ni mwelewa sana anataka mabadiliko ameifanya elimu kuwa kipaumbele kwenye serikali yake siamini kwamba tukimpa wazo hili atalikataa".

Alisema Chuo Kikuu Zanzibar (SUZA) kinachangamoto kubwa ya nafasi na uwezo wake ni kuchukua wanafunzi 60 kwenye kozi ya afya lakini wanaomba kusoma masomo hayo ni zaidi ya 800.

"Tunashindwa kuwachukua kwasababu hatuna sehemu ya kuwaweka na kwa maana hiyo tunakosa wataalamu wengi wa sekta ya afya, hivyo kuna umuhimu wa kuwapeleka nje ya nchi ili tupate wataalamu wengi wa fani ya afya," alisema.

Pia alisema Rais Hussein Mwinyi anatoa nafasi za vijana kwenda kusoma nje ya nchi, hivyo ni wakati mwafaka kwenda kumshauri kuwapeleka nje wale ambao wanakosa nafasi kwenye fani wanazoomba hapa nchini.

Alisema hivi karibuni Baraza la Wawakilishi litaanza vikao vyake hivyo, atatumia nafasi yake kuitambulisha Global kwa wajumbe wa baraza hilo, ili waweze kuwafahamu na wawatumie kwa ajili ya kupeleka watoto wao nje.

Mkurugenzi Mkuu wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema Rais Dk. Hussein Mwinyi amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha uwekezaji kwenye uchumi wa buluu na maono makubwa ya kukuza uchumi wa Zanzibar, hivyo kuna umuhimu wa kufanya maandalizi mazuri ya rasilimali watu.

# CHADEMA yakamia jimbo la Chato kwa hali na mali

**Elizabeth Zaya na Enock Charles**




CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeeleza nia yake ya kulitwaa Jimbo la Chato kwa kushinda viti vingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na ule wa ubunge na madiwani mwakani.

Jimbo hilo ambalo kwa muda mrefu tangu likiwa Biharamulo Magharibi mwaka 1995 hadi lilipoitwa Chato baada ya kuanzishwa wilaya, lilikuwa chini ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli mpaka mwaka 2015 na baada ya hapo Dk. Medard Kalemani mpaka sasa.

Mwenyekiti wa Kanda ya Victoria, Hezekiah Wenje, ambaye anawania tena nafasi hiyo, alisema jana kuwa Chato ni moja ya majimbo yaliyoko katika kanda hiyo ambayo wamepania kushinda yote katika uchaguzi ujao.

"Kwa kanda nzima ya Victoria katika majimbo 25, mpango wetu ni kupata majimbo si chini ya 16 likiwamo la Chato na uwezekano upo. Tumeshafanya tathmini na utafiti wa kutosha.

"Kwa mfano Jimbo la Chato tumewahi kuongoza serikali za vijiji vingi kuliko Chama Cha Mapinduzi (CCM) tena kipindi cha Magufuli," alisema.

Wenje alisema hiyo ni miongoni mwa mikakati yake endapo atateuliwa tena kugombea kanda hiyo na kuitetea kwa mara nyingine.

Kamati Kuu ya CHADEMA iliyoketi Dar es Salaam tangu mwishoni mwa wiki iliyopita, ilihitimisha vikao vyake jana ambavyo pamoja na mambo mengine, ilifanya usaili wa wanaoomba nafasi za uongozi katika kanda.

Katika hatua nyingine, baadhi ya viongozi wa CHADEMA wameeleza matumizi ya jengo jipya la ofisi za chama hicho, Mikocheni, Dar es Salaam, yalivyopunguza gharama ambazo zingetumika katika kikao cha kamati kuu. Kwa mara ya kwanza, chama hicho kilitumia jengo hilo ambalo kilinunua tangu mwaka jana.

Mara kadhaa, chama hicho kinapokuwa na vikao vya kamati kuu, kilikuwa kikijichimbia kwenye hoteli za kifahari katika mikoa mbalimbali, hasa Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Itifaki na Mawasiliano kwa Umma, John Mrema, alisema kwa kutumia ofisi hiyo mpya, kuna gharama kubwa wameokoa lakini pia wamepata utulivu mzuri wa kujadili hoja mbalimbali.

"Ni kweli kuna gharama zinapungua. Ukikaa kwenye hoteli huko ukichukua mkataba wanakwambia mpaka saa fulani mwisho lakini ukikaa hapa hata tukimaliza saa 7:00 usiku hakuna mtu wa kutubughudhi.

"Baada ya kumaliza kikao hiki tutakaa tupige hesabu zilizotumika hapa halafu tulinganishe na zile ambazo tumekuwa tukitumia kwenye vikao kama hivi tukifanyia hotelini," alisema.

Frank Mwakajoka anayetia nia katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti Kanda ya Nyasa, ambaye aliwahi kuwa mbunge wa Tunduma, alisema wazo la kufanyia vikao katika ofisi hizo ni jema kwa sababu wanaamini kwamba fedha iliyookolewa kwa kutokufanyia katika hotelini ni kubwa na itafanya kazi zingine za chama.

Naye Ezekiel alisema: "Ni salama zaidi na imepunguza gharama kwa kiasi kikubwa. "Kwa akili ya kawaida tu ni lazima gharama zimepungua tena nyinyi. Mnajua viwango vyetu tulikuwa tukikodi ukumbi mara Bahari Beach mara wapi lakini sasa tuko katika ofisi zetu.

"Hata kiusalama pia ni uhakika kwa sababu haya ni majengo yetu hatuna wasiwasi kwamba mtu anaweza kukuwekea kakitu kwa chini hivi na tuna CCTV camera za kwetu kwa hiyo hakuna wasiwasi."

# DMO atwishwa zigo madai wajawazito kutozwa fedha

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, amemwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo (DMO), Dk. Zelha Hamza, kufika katika Zahanati ya Bonyokwa kufuatilia madai ya baadhi ya wajawazito kutozwa Sh. 30,000 wanapokwenda kupata huduma.

Mpogolo alitoa agizo hilo juzi jijini Dar es Salaam, katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Diwani wa Bonyokwa, Tumike Malilo, kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Agizo hilo lilitokana na baadhi ya kinamama kuwasilisha kero wakidai kitendo hicho kinasababisha wasio na uwezo kifedha kukosa huduma za afya ya uzazi.

"Sera ya serikali matibabu kwa mjamzito ni bure. Ninamshangaa huyo anayetoza hela. Nitafuatilia leo (juzi) hii. Majamzito ni bure na mtoto chini ya umri wa miaka mitano bure. Ninamwagiza DMO afike katika zahanati hiyo na kutatua tatizo hilo," alisema.

Alisema huduma bure kwa mjamzito ni suala lililoamuriwa na serikali kwa makusudi na pia ni sera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Diwani Malilo alisema katika kata hiyo, kero nyingi zimetatulia na zilizosalia zinatafutiwa ufumbuzi.

"Barabara ya kwenda zahanati ilishatengenezwa kwa kiwango cha zege, kimebaki kipande kidogo nacho kiko tayari kwenye mpango wa kumaliziwa mwaka huu.

"Ile ya kutoka Kinyerezi hadi Bonyokwa mapaka Kimara tayari mkandarasi yuko 'site' (kazini). Mvua itakapoisha ataanza kazi. Kuna barabara ya kutoka Masia, Kanisa Katoliki mpaka Baa Mpya iko katika mpango wa kujengwa.

"Lakini pia ya kutoka Segerea kwenda Bonyokwa tayari imejengwa mita 700 kwa kiwango cha lami na kipande kilichobaki kimeingia katika bajeti ya mwaka 2024/25 nacho kitamaliziwa mpaka kufika mwakani barabara nyingi zitakuwa zimejengwa," alisema Malilo.

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 itakapoanza kutolewa ili kujikwamua kimaisha.

"Mikopo muda si mrefu itaanza kutolewa, hvyo niwaombe mchangamkie mjiunge katika vikundi, fungueni akaunti benki mkajisalili ili iwe rahisi kupata mkopo. Tatizo kinamama wengi hawataki kufuata huo utaratibu ndiyo maana wanaangukia katika mikopo ya kausha damu," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Kisiwani – Bonyokwa, Peter Mwasingi, alitumia mkutano huo kuwaaga wanakata wake kwamba hana nia tena ya kugombea katika nafasi hiyo, akisisitiza anataka kustaafu.

Alikumbushia kuwa wakati anaingia madarakani aliukuta mtaa huo una changamoto kadhaa zikiwamo maji, barabara na daraja na kwamba anamshukuru Mungu kwa kushirikiana na serikali yote yametatuliwa.

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**ADEEL KHALID HAJEE** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu Khalid Adam Hajee anatangaza kupotelewa na hati ya nyumba, Plot Na. **1 Kitalu 2L** iliyoko Wilaya ya **Handeni kata ya Chanika**. Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **HAN/B.1/1/19/VOL.1/169.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALEEM SULTAN VIRANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0335-0081** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AGAKHAN MZIZIMA SEC SCHOOL** mwaka 1997. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/87874/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ALICE PATRICK LIHUNDI** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili **MC 141 CDH na MC 446 CMF.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Control No. **9910841100922.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TRELA

**ELISAFINA ELISANTE CHIZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **Trela** yenye namba za usajili **T 133 DCX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/SHI/KAH/2971/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRIDAH CHARLES RIZIKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0493-0014** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ALHARAMAIN ISLAMIC HIGH SCHOOL mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MTW/MTW/2333/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA TARAKA NAMBA:-...13.2024**

**MUOMBAJI:- JASTIN FAUSTIN NYONI**

**DHIDI YA**

**MDAIWA:- JUDITH RAFAEL LUKASI**

**Kwa:- JUDITH RAFAEL LUKASI**

**Ombi la Muombaji:- JASTIN FAUSTIN NYONI. Madai ya TALAKA**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 20 Mwezi 05 Mwaka 2024 Saa 8:30 Asubuhi /alasiri.
Angalia kama *hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kitoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 05. 2024.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOYCE SHEDRACK KASANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 380 CCG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/GEI/MBO/2909/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 9058 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FRANK ELIYA MGAYA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARIA ANTHONY MSINDAI**

**GENERAL CITATION (Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 24th day of May 2024

Dated at Korogwe this **06th day of May 2024**

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 10929/2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MARIAM AHMED PATEL**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY THABIT MZOMOZI...................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22nd day of May, 2024
Dated at Kyela this 13th day of May, 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

HABARI MAALUM

# Mhariri Mtendaji wa Nipashe ashinda tuzo kimataifa uongozi katika habari

**Na Salome Kitomari**

MHARIRI Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, ametangazwa kuwa mshindi wa tuzo ya Mwanamke Kiongozi katika Chombo cha Habari (2024 Women In News Laureate Leadership Awards), iliyotolewa na Umoja wa Wachapishaji wa Magazeti Duniani (WAN-IFRA).

Akitangaza washindi wa tuzo hiyo kwa mwaka huu, Melanie Walker, Mkurugenzi Mtendaji wa WAN-IFRA anayeshughulikia Maendeleo ya Vyombo vya Habari na Programu ya Wanawake Katika Habari (Women in News), alisema tuzo hiyo hutolewa kwa wanawake viongozi ndani ya vyumba vya habari waliotoa mchango wa kipekee kwenye sekta na uhuru wa habari, usawa wa kijinsia na kujenga kizazi kijacho cha viongozi.

Alisema Beatrice kwa zaidi ya miaka 25 katika tasnia ya Habari, ameongoza jitihada katika kupinga ukatili wa kijinsia kupitia vyombo vya Habari, hivyo kutoa mchango makini ulioleta mabadiliko.

Akizungumza katika mahojiano maalum kuhusu tuzo hiyo, Bandawe ambaye amekuwa kwenye taaluma ya habari kwa zaidi ya miaka 30, alisema amepokea kwa furaha kwa sababu ni mara ya kwanza kwa Tanzania kupokea baada ya nchi za ukanda wa Afrika za Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe na Botswana.

"Najisikia faraja kubwa sana kwanza Kampuni ya The Guardian Limited iliniamini kwa kunipa uongozi, nimejitahidi kwa uwezo wangu hadi nimetambuliwa kimataifa, nilichokifanya ni mchango wangu kama kiongozi kuhakikisha maudhui ya taarifa zetu yanazingatia usawa wa kijinsia.

"Mara nyingi habari tunazochapisha hazitoi fursa ya sauti nyingine kusikika, lakini tumeweka utaratibu maalum kwenye chombo chetu kwamba habari zote lazima ziwe jumuishi ili matatizo ya jamii yaweze kufanyiwa kazi," alisema.

Alipoulizwa ni mambo gani anafikiri yamemfanya awe mshindi, alisema: "Kama kiongozi si kazi yako kuwapangia kazi tu unaowasimamia bali uwaongoze ili nao waje kuwa viongozi kwenye vyombo vya habari. Kuna ombwe kwenye vyumbo vya habari kuwa na viongozi wanawake kwani wengi ni wanaume," alisema.

Kutokana na tuzo hiyo, aliwataka wanawake na wasichana walioko kwenye uandishi wa habari kutokubali kukatishwa

tamaa na mazingira au maneno kwa kuwa unapokuwa kwenye uongozi kuna mambo mengi.

"Unapokuwa kwenye ngazi ya juu unaweza kukatishwa tamaa. Utaambiwa huna uwezo, hu-



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe akiwa katika mazungumzo na mmoja wa waandishi wa gazeti hili. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

> Naipongeza timu yangu wamenipa ushirikiano mkubwa. Tunasikilizana, nasikiliza mawazo yao na nimekuwa nikishirikiana nao kwenye mambo ya kazi na nje ya kazi.

fai kuongoza. Hivyo vyote visikufanye upoteze mwelekeo wa kufanya kazi kwa bidii. Wako watakuona na wataona mafanikio yako, lakini ukikata tamaa wanaokuangalia nao watakata tamaa wataona kuna ugumu huwezi kutoboa, hivyo hutasaidia wanawake kuwa viongozi," alisema.

Kuhusu nyakati ngumu amewahi kuzipitia kwenye uongozi na aliwezaje kuvuka salama, alisema; "Ni siku nilipoteuliwa kuwa Mhariri Mtendaji kwa sababu nilipokea uteuzi wakati watangulizi wangu hawakuwa wameondoka vizuri.

"Ilikuwa tofauti na vyeo nilivyopewa huko nyuma unafurahia kupata nafasi ya juu. Niliona nimebeba mzigo mkubwa, lakini nilisimamia misingi ya kazi tangu 2018 hadi sasa niko kwenye nafasi hii.

"Wakati mgumu ni pale ambapo unatoa habari alafu inakuwa haijazipendeza mamlaka. Unaitwa unahojiwa, inakuumiza na kukuweka katika wakati mgumu. Lakini kama unasimamia misingi ya kazi, haiwezi kukusumbua kwa kuwa utajitetea na maisha yataendelea."

Bandawe alisema ushindi huo si wake peke yake bali wa timu nzima ya The Guardian ambayo imempa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kwa kuwa hafanyi kazi hizo pekee yake.

"Naipongeza timu yangu wamenipa ushirikiano mkubwa. Tunasikilizana, nasikiliza mawazo yao na nimekuwa nikishirikiana nao kwenye mambo ya kazi na nje ya kazi," alisema.

Alama anazoziona kwenye taaluma ya habari tangu aingie, alisema: Ninazoziona ni uchapakazi, sijisifii ila nikipewa kazi naifanya kwa uwezo wangu wote. Hii imetoa nafasi kwa wenzangu wote walio chini yangu na ushirikiano na wenzangu sehemu ya kazi na nje ya kazi. Imesaidia sana kuweka ukaribu, mtu hafikiri mara mbili kunifikia na kuomba ushauri na kueleza jambo lake."

Hata hivyo, alisema tunzo hiyo ni kwa ajili ya wanawake walioko kwenye vyumba vya habari kwa sababu ya uchache wao na lengo si wanawake wawe bora zaidi ya wanaume bali kuwe na usawa na ujumuishi ili sauti zote zisikike katika jamii.

Bandawe aliwashauri wamiliki wa vyombo vya habari wazingatie usawa wa kijinsia na si kuangalia wingi wa wanawake lakini na uwezo wao kama ilivyoainishwa katika Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDG) ya 50 kwa 50.

"Ni lazima tuangalie wanawake walioko kwenye vyombo vya habari. Kampuni ya IPP Media ni mfano mzuri kwa sababu viongozi wake wengi ni wanawake. Kuanzia ITV, The Guardian Limited na EATV kuna wanawake ngazi ya uamuzi na hiyo inasaidia kuongeza ujumuyishi," alisema.

Aidha, aliwashauri wanawake na wasichana walioko kwenye taaluma ya habari kuendelea kufanya kazi kwa bidi kwa kuwa ni fani nzuri inayowakutanisha na watu wengi, kusafiri sehemu tofauti ndani na nje ya nchi ikiwamo kujifunza mambo mengi. Kwa mantiki hiyo, alisema ni muhimu wazazi kuruhusu watoto wao kusoma fani hiyo.

**SAFARI YAKE**

Bandawe aliingia katika fani ya habari akiwa mwandishi, baadaye mwandishi mwandamizi, Mhariri wa Habari, Mhariri wa Habari za mikoa, Mhariri Weekend na sasa ni Mhariri Mtendaji.

Tuzo ya 2024 Women in News Laureate Leadership Award imetolewa kwa wanawake viongozi ndani ya vyombo vya habari katika ukanda wa Afrika, Asia na Uarabuni.

Washindi wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa AJ+, Dima Khatib nchini Palestine/Syria na Mkurugenzi na Mhariri Mkuu, Nan Paw Gay wa Karen Information Center, Myanmar.

"Huu ni ushindi wa kupigiwa mfano kwa viongozi walionyesha mfano na kujitoa kwa ubora wa uandishi wa habari, kuwa mfano wa kuigwa kwa wengine na kuleta mabadiliko chanya kwenye nchi zao na zaidi," alisema Vincent Peyrègne, Mtendaji Mkuu wa WAN-IFRA.

"Tunajivunia mafanikio haya makubwa na ni heshima kwa waandishi wa habari ambao wametoa uongozi bora na uvumilivu hasa kwa wakati huu ambao vyombo vya habari vinakabiliwa na changamoto nyingi," alisema.

Bandawe, Khatib and Paw Gay watatambuliwa kwenye Kongamano la Dunia la WAN-IFRA (World News Media Congress), litakalofanyika Copenhagen, Denmark kuanzia Mei 27-29, mwaka huu.

# NYOTA YANGA 'WALILIA' HATIMA MTIBWA SUGAR

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI wakishuhudia timu yao ikiitwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1, nyota wa Yanga, Dickson Job na Kibwana Shomari, wameonyesha hisia zao kwa timu yao ya zamani, Mtibwa Sugar ambayo inaburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Wakizungumza na gazeti hili, nyota hao ambao wameichezea Mtibwa Sugar kabla ya kusajiliwa na Yanga, wameonyesha huzuni kutokana na hali wanayoipitia wachezaji wa timu hiyo inayopambana kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Job aliliambia gazeti hili anajisikia vibaya kuona Yanga imeendelea ‚kuzamisha' jahazi la timu hiyo ambayo ilimkuza na kumtambulisha katika ulimwengu wa soka la Tanzania.

„Ni matokeo mazuri kwetu, mchezo huu ulikuwa mgumu sana kwangu, kwanza tulihitaji matokeo yatakayotufanya tutangaze ubingwa, lakini pia Mtibwa ilihitaji matokeo ya kuweka hai matumaini yao ya kubaki Ligi Kuu, sikuwa na namna kwa sababu hii ni kazi na ilikuwa lazima kusaka ushindi, nawasikitikia Mtibwa lakini naamini wanaweza kupambana wakabaki Ligi Kuu," alisema Job.

Aliongeza Mtibwa Sugar wanaweza kupambana katika michezo iliyobakia na kujihakikishia tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao na kukwepa kushuka daraja.

Naye Kibwana alisema anasikia ‚maumivu' kuona Mtibwa Sugar ikiwa katika hali ngumu kwa sababu ni ‚Chuo cha vijana' wengi kwenye soka hapa nchini.

„Vijana wengi wamepita Mtibwa kama ilivyokuwa kwangu, ni timu inayotoa fursa kwa vijana kufikia ndoto zao, mimi nawatakia heri wapambane katika michezo iliyobaki na kuona kama watabaki Ligi Kuu, ushindi tulioupata Yanga dhidi yao ni mzuri kwangu lakini pia unanipa majonzi kuona tumeididimiza Mtibwa," alisema Kibwana.

Ushindi wa juzi umeifanya Yanga kufikisha pointi 71 ambazo hazitafikiwa na timu nyingine msimu huu na hivyo kutangaza ubingwa wake wa 30 wa Ligi Kuu Tanzania Bara lakini umeifanya Mtibwa Sugar kukaribia kushuka daraja msimu huu.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (wa pili kushoto), akimkabidhi bendera ya Taifa Nahodha wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa wenye Ulemavu 'Tembo Warriors', Juma Kidevu (kulia), inayokwenda Misri kushiriki mashindano ya wenye ulemavu Afrika, makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam FC 'yaota' nafasi ya pili

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema kwa sasa timu yake inajipanga kuhakikisha inamaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na pia kutinga fainali ya mashindano ya Kombe la FA.

Dabo ameliambia gazeti hili hayo ndio mambo mawili muhimu yanayotizamwa na kikosi chake na watapambana kuhakikisha wanavuta pointi tisa katika michezo mitatu iliyobakia msimu huu, miwili wakicheza ugenini dhidi ya JKT Tanzania na Geita Gold FC na mmoja watakuwa nyumbani kuwakaribisha Kagera Sugar.

Kabla ya michezo hiyo Azam FC atakuwa na kibarua cha kuikabili Coastal Union katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA itakayochezwa Mei 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kocha Dabo huyo alisema anafahamu kuna ushindani katika nafasi ya pili kwa sababu ya kujihakikishia tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

„Tunahitaji kucheza fainali ya FA, ili kufikia malengo hayo lazima tumfunge Coastal Union, ninaimani kila kitu kinawezekana kuhusu fainali matumaini yapo inategemea na sisi," alisema Dabo.

Aliongeza wamekuwa na wakati mgumu kwa kucheza mechi kila baada ya siku tatu na akaongeza hana kikosi kipana kwa sasa kutokana na idadi kubwa ya wachezaji wake ni majeruhi.

„Lakini tunaendelea kuwa bora na kujifunza, kama kocha na wachezaji hii ni hali mpya kwetu na kila muda tunahitaji kupata somo na kuwa shupavu kila siku baada ya siku, tuna siku chache kuanzia leo na siku zijazo za mechi," Dabo aliongeza.

## KMKM, KVZ zatupwa nje mashindano FA Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KMKM SC na KVZ FC zimetupwa nje katika mashindano ya Kombe la ZFF (FA CUP), baada ya kushindwa kung'aa katika mechi zao za hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

KMKM imeondolewa na Wanajeshi wa Mipakani Uhamiaji FC kwa kuchapwa mabao 4-0 wakati KVZ walifungwa na Mlandege penalti 4-3 kutokana na kutoka sare dakika 90 za kawaida.

Kocha Mkuu wa KVZ, Ali Mohmmed Ameir, alisema halikuwa lengo lao kuishia hatua hiyo katika michuano hii licha ya wachezaji wake kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo huo.

"Mchezo wenyewe tangu unaanza ulikuwa mgumu wa hali juu, wapinzani wetu walikuja na mpango wa kuhakikisha wanasonga mbele, mpango ambao ulikuwa sawa na wetu, lakini kama tunavyojua penalti huangukia kwa mwenye bahati," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa wanaelekeza nguvu zao zote katika michezo saba ya Ligi Kuu Zanzibar iliyobakia na wataendelea na vita ya kuwania taji hilo kwa sababu bado ubingwa hauna mwenyewe.

## Mbeya wanawake kuchaguana Juni 13

**Na Somoe Ng'itu**

CHAMA cha Mpira wa Miguu wa Wanawake Mkoa wa Mbeya (MRWFA), kinatarajia kufanya uchaguzi mkuu ifikapo Juni 13, mwaka huu imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mbeya (MREFA), John Stephen, alisema mchakato wa kutoa fomu kwa wagombea ulianza rasmi juzi na utamalizika keshokutwa.

Alitaja nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni Mwenyekiti, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TWFA na Wajumbe wawili wa Kamati ya Utendaji.

„Tunawaomba wadau wenye sifa kujitokeza kuwania nafasi za uongozi ili kulisukuma soka la wanawake Mbeya," alisema mwenyekiti huyo.

Wakati huo huo, Uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Miguu wa Wanawake Mkoa wa Simiyu umepangwa kufanyika Mei 24, mwaka huu mkoani huko.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi wa chama hicho, Gloria Ikanda, alisema wagombea watakaopitishwa watatakiwa kuanza kampeni za kujinadi kuanzia Mei 20, mwaka huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO ATAKIWA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu ya Saudia (Saudi Pro) zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil Casemiro mwenye umri wa miaka 32 na kiungo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 29 Bruno Fernandes. (***Telegraph***)

### WALTERS AIKATALIA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kumpoteza mlinzi Reuell Walters mwenye umri wa miaka 19, baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kukataa ofa ya mkataba mpya ili kutafuta nafasi kwingineko. (Athletic)

### TRENT AWINDWA REAL MADRID

REAL Madrid bado wana nia ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 25 kutoka Liverpool. (***Fabrizio Romano kupitia Football365***)

### MBAPPE HAKUNA MZOZO

RIPOTI za kuibuka kwa mzozo mkubwa kati ya mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe mwenye miaka 25 na Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi kabla ya mechi ya Ligue 1 dhidi ya Toulouse zimetupiliwa mbali na vyanzo vya mabingwa hao wa Ufaransa. (***Marca***)

### ALONZO AZITAKA ZOTE TATU

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso anatumai kusimamia klabu zake zote tatu za zamani za Liverpool, Real Madrid na Bayern Munich lakini hana uhakika ni kwa utaratibu gani. (***Abendzeitung***)

### BAYERN YABANIWA GLASNER

NIA ya Bayern Munich kumnunua kocha wa Crystal Palace, Oliver Glasner ilififia baada ya klabu hiyo ya Bundesliga kuambiwa itawagharimu pauni milioni 86. (***Bild***)

### CONTE ANUKIA NAPOLI

KLABU ya Napoli imeanzisha tena mazungumzo na Antonio Conte kuhusu kuwa kocha wao baada ya Muitaliano huyo kupunguza mahitaji yake ya mshahara huku AC Milan pia ikitaka kuzungumza na kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Tottenham. (***Il Mattino***)

### RAMOS KUHAMIA MAREKANI

MLINZI wa zamani wa Sevilla na timu ya taifa ya Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 38, amepiga hatua katika mazungumzo yake na klabu ya San Diego FC kuhusu kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS). (***Athletic***)

### ASHLEY COLE ANYATIWA

BEKI wa zamani wa timu ya taifa ya England na klabu za Ligi Kuu ya England Arsenal na Chelsea, Ashley Cole mwenye umri wa miaka 43, ananyatiwa na klabu kadhaa za Championship ili kuchukua nafasi ya ukocha. (***Mirror***)

### CHELSEA KUSAJILI MABEKI

KLABU ya Chelsea inatazamia kusajili mshambuliaji na mabeki wawili msimu huu wa majira ya joto huku wakurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Paul Winstanley na Laurence Stewart wakitarajiwa kukabidhiwa tena majukumu yao ya uhamisho. (***Telegraph***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCELONA YATAJA BEI YA RONALD ARAUJO

●●● Nyota huyo anatakiwa na vigogo wakubwa wawili wa soka la Ulaya na sasa...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeweka bei inayotakiwa ya euro milioni 100 kwa Bayern Munich na Manchester United wanaomwania nyota wa timu hiyo, Ronald Araujo, kulingana na ripoti nchini Hispania.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa akiongeza kiwango chake cha uchezaji mara kwa mara baada ya kupanda kutoka timu B ya Barcelona mwaka 2020 na anachukuliwa kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi kwenye La Liga.**

Araujo amecheza nafasi ya beki wa kati mwandamizi msimu huu, huku kijana, Pau Cubarsi akipanda hadi kwenye kikosi cha kwanza mara kwa mara, lakini mustakabali wake wa muda mrefu katika klabu hiyo ya Kalalunya haujulikani.

Bayern na United wamekuwa wakihusishwa kwa kiasi kikubwa kutaka kumnunua Araujo ambaye mkataba wake na Barcelona unamalizika 2026, ingawa raia huyo wa Uruguay alikanusha ripoti za uwezekano wa kuhama Machi kabla ya kurudia Aprili kwamba mazungumzo kuhusu mkataba mpya yanakwenda vizuri.


Hata hivyo, uvumi kwamba Barcelona ambao wana uhaba wa fedha wanaweza kutaka kumuuza Araujo ili kuimarisha kikosi chao unaendelea kutawala safu za uvumi kote Ulaya, huku Frenkie de Jong, Robert Lewandowski na Raphinha wachezaji wengine watatu wakitarajiwa kuondoka majira ya kiangazi.

Chapisho la gazeti la Sport limeripoti kwamba Barcelona wanamthaminisha Araujo karibu na euro milioni 100 na ripoti yao imeiweka Bayern kama watu wanaopewa nafasi kubwa ya kukamilisha uhamisho huo msimu huu wa majira ya joto.

Bavaria hao wanasemekana kuwa na nguvu ya kifedha ya kumpa mshahara ,wa kuvutia' Araujo ambaye kuuzwa kwake kunaweza kuisaidia Barcelona kupata fedha za kusajili wachezaji wapya kwenye safu ya kiungo wa kati au fowadi.

HABARI MICHEZO

# SOUTHGATE APATA KIGUGUMIZI KUBAKI AU KUONDOKA ENGLAND



**LONDON,** England

KOCHA wa England, Gareth Southgate amesema Kombe la Dunia la 2026 litakuwa „mashindano ya kustaajabisha“ lakini akakataa kuthibitisha kama atasalia katika wadhifa wake zaidi ya mwaka huu.

Mkataba wa kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 unamalizika Desemba mwaka huu, na vyanzo viliiambia ESPN kwamba Chama cha Soka kinatamani Southgate abaki kuinoa timu hiyo kwa kuwaongoza ‚Simba Watatu‘ hao kwenye Kombe la Dunia la kwanza la timu 48, litakalofanyika nchini Marekani, Mexico na Canada.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Southgate anafikiriwa sana kuchukua nafasi ya Erik ten Hag iwapo Manchester United itaamua kumfukuza kocha huyo Mholanzi katika wiki zijazo.

Southgate alihuzunishwa na mustakabali wake baada ya England kutolewa katika robo fainali na Ufaransa kwenye Kombe la Dunia la 2022 kabla ya kukubaliana na mkataba mpya zaidi ya michuano ya Ulaya mwaka huu nchini Ujerumani.

Katika mahojiano ya kipekee na ESPN, Southgate alisema: „Nadhani ‚2026 itakuwa Kombe la Dunia la ajabu. Nina umri wa kutosha kukumbuka mwaka 1994 nchini Marekani.

„Lakini unajua kwamba tukio lolote la michezo Marekani inashiriki katika kuandaa na ni wazi Mexico 1986 pia ninakumbuka hayo yatakuwa mashindano ya kushangaza, ambayo yatakuwa na aina tofauti ya changamoto.

„Ikiwa unafikiria kuhusu usafiri na maeneo ya saa ikilinganishwa na Kombe la Dunia lililopita, haiwezi kuwa tofauti zaidi. Mabadiliko ya joto na kitu ambacho unaweza kukabiliana nacho. Hivyo hayo pia yote yatafanya mashindano haya kuwa ya kushangaza.“

Alipoulizwa kama atashawishika kubaki, Southgate alisema: „Hiyo itategemea kucheza vizuri, kupata matokeo na kutaka kubaki. Idadi yoyote ya mambo itamalizwa katika hilo. Lakini hiyo ni ya baada ya majira haya ya joto.“



# Rooney awashutumu wachezaji Man United

**MANCHESTER,** England

GWIJI wa Manchester United, Wayne Rooney, amewashutumu wachezaji wa kikosi cha Erik ten Hag kwa kujificha nyuma ya majeraha na kuchagua kutoshiriki katika timu yao mwishoni mwa msimu huu.

Ukosoaji wa mshambuliaji huyo wa zamani umekuja baada ya United kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Arsenal kwenye Uwanja wa Old Trafford, wakati ambapo kocha Ten Hag alilazimika kukabiliana na wachezaji wengi waliokosekana huku Marcus Rashford na nahodha Bruno Fernandes wakishindwa kujumuishwa kwenye kikosi.

Kukosekana kwao kunaongeza orodha inayoongezeka ya wachezaji majeruhi wa United, huku Mason Mount, Harry Maguire, Luke Shaw, Raphael Varane, Lisandro Martinez, Victor Lindelof, Tyrell Malacia na Anthony Martial wakiwa nje kwa sasa.

Rooney alikuwapo kwenye mechi ya Jumapili waliyopoteza Old Trafford, alitoa mawazo yake kuhusu shida ya timu yake ya zamani.

Akizungumza na Sky Sports alisema: “Kikosi kina wachezaji wazuri sana lakini uchezaji wao uko chini ya kiwango, tukiangalia majeruhi waliopoa bado baadhi ya wachezaji waliopo wanaweza kucheza kwa asilimia 100.

„Kama wako nyuma ya Ten Hag hawaoneshi vizuri sana. Ni rahisi unapokuwa na Ubingwa wa Ulaya au fainali ya Kombe la FA, kwa wachezaji kukaa nje kwa muda kidogo kisha wajiandae na fainali na Euro.

„Nimejionea hili kwa miaka mingi na nadhani wachezaji hawajijazi na sifa yoyote kwa sasa na makocha wanawajibika kwa hilo.“



# Diaz adokeza juu ya mustakabali wake

**LIVERPOOL,** England

LUIS Diaz amekiri kwamba anafurahishwa na nafasi yake katika klabu ya Liverpool huku kukiwa na tetesi zinazomhusisha na kuondoka Anfield msimu huu wa majira ya joto.

Winga huyo wa Colombia amekuwa sehemu muhimu ya kikosi cha Jurgen Klopp tangu ajiunge na timu hiyo Januari 2022.

Amefunga mabao 13 katika michuano yote msimu huu na kuwindwa na timu mbalimbali za Ulaya.

Jina la Diaz limekuwa likitajwa mara kwa mara kutaka kujiunga na PS hasa katika kipindi hiki ambacho nyota wa timu hiyo, Kylian Mbappe akitangaza mpango wake wa kuondoka katika klabu hiyo ya Ligue 1.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hata hivyo, anaweza kuendelea na soka lake Anfield, mkataba wake wa sasa hautakamilika hadi 2027, na hivi majuzi alisisitiza kuwa kwa sasa hafikirii maisha ya mbali na Liverpool.

Katika mahojiano na vyombo vya habari vya klabu, Diaz alisema: „Nimekua sana. Tangu mwanzo wa kazi yangu hadi sasa, ninahisi kwamba kwa siku, miaka, kuishi kila uzoefu katika kila timu tofauti, kuja kwenye hii klabu hii kubwa ya Liverpool, inakuacha na mambo mengi ya kujifunza.

„Unajifunza zaidi na zaidi kuwa mtaalamu, kuwa mtu bora, kuwa mchezaji mzuri na mtu mzuri. Ukweli ni kwamba nina furaha sana kuwa hapa. Miaka mingi inakuja kwa klabu.

„Binafsi, siku zote nitajaribu kufanya niwezavyo, siku zote nitajaribu kujitoa kwa asilimia 100, ili kujitokeza uwanjani kila mara, jambo ambalo nilikuja hapa kulifanya. Ninamshukuru Mungu kila mara kwa kila nafasi.“

Liverpool wanajipanga kumkaribisha kocha mpya Arne Slot katika timu hiyo, huku kocha maarufu Klopp akijiuzulu wadhifa wake mwishoni mwa msimu huu.

Msimu wa mwisho wa Klopp unaweza kukosa ‚utukufu‘, lakini Diaz anaamini bado kuna mambo ya kuchukua katika kampeni zao msimu huu.

„Kwetu sisi, ilikuwa muhimu kushinda ligi na mashindano yote tuliyokuwa nayo,“ Diaz alisema kuhusu kuaga kwa Klopp.

„Kwa bahati mbaya, matokeo hayakuweza kupatikana hivi majuzi. Tulianguka kama timu, lakini tulifanya msimu mzuri, kibinafsi na kama timu, kuna mambo mengi ya kuboresha ili tuwe na msimu mzuri. Lakini nina furaha na nimeridhika kuwa hapa.“

## Simba Queens yasaka rekodi

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kukaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens inataka kumaliza msimu huu bila ya kufungwa mechi hata moja.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan ‚Mgosi' ameliambia gazeti hili anataka kushinda mechi zote zilizosalia na hatawadharau wapinzani wao kwa sababu anataka kuweka rekodi ya kutopoteza mchezo.

Mgosi alisema wanaheshimu kila timu wanayocheza nayo na kwao kila mechi ni sawa na fainali.

„Tunataka kushinda mechi zote, tunataka kumaliza msimu na rekodi nzuri, hatutabweteka, tunataka kushinda michezo iliyobakia, tunaendelea kujipanga ili kuhakikisha tunafikia malengo," Mgosi alisema.

Bingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ataiwakilisha Bara katika mashindano ya kimataifa ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika baadaye mwaka huu.

JKT Queens ya Tanzania Bara ndio ilikuwa inashikilia ubingwa wa CECAFA ambao iliwavua Simba Queens msimu uliopita, lakini Maafande hao walishia hatua ya makundi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa wanawake.

# MGUNDA AIPONGEZA YANGA, AWAFUNDA BALUA, CHASAMBI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, akiipongeza Yanga kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, amesema kwa sasa yupo katika darasa la ‚kuwafunda' nyota wake, Freddy Michael, Edwin Balua na Ladack Chasambi, kwa lengo la kusaidia timu kupata matokeo chanya.

Freddy alikosa mabao ya wazi katika mechi dhidi ya Kagera Sugar huku Balua na Chasambi, wao wanatakiwa kucheza kitimu zaidi na kuacha ubinafsi.

Akizungumza na gazeti hili baada ya timu yake kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Kagera Sugar, Mgunda alisema yeye kama mwanamichezo, anaipongeza Yanga kwa sababu imeshatangazwa kuwa mabingwa.

„Nchi yote imeshajua wamekuwa mabingwa, yote kwa yote hii ni michezo, tuwapongeze, wameshatangaza ubingwa, ni jambo jema, nadhani mbio za ubingwa zimeshaisha, sasa tuendelee na mbio zetu na tuombeane heri," alisema Mgunda.

Kuhusu mechi dhidi ya Kagera Sugar, Mgunda alisema mashabiki wengi walionyesha kutoridhishwa na Freddy ambaye alikosa mabao mawili ya wazi, lakini pia walionekana kuwakosoa nyota vijana, Chasambi na Balua kwa tabia ya ubinafsi iliyopelekea kuikosesha timu kufunga mabao rahisi katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema suala hilo tayari ameshaanza kulifanyia kazi kwa kuwaandalia mafunzo maalumu na anaamini hayatajirudia.

„Kwa upande wa Freddy nimekaa na mchezaji mwenyewe, nimemweleza nini cha kufanya siku nyingine ukija mpira kama ule usifanye hivi, unatakiwa kufanya hivi. Sisi kama walimu ambao tumecheza soka tunajua sababu ni nini, na tunataka kumrekebisha ili baadaye tujue tatizo ni yeye mwenyewe, au huwa hajiweki sehemu nzuri.

Lazima tuamini hakuna straika ambaye ananuia kutofunga, inapotokea huwa na sababu, ama za yeye mwenyewe, au anapofika langoni anakuwa bado hajajiandaa kumaliza kazi ya kuuweka mpira wavuni, hiyo sisi ndiyo kazi yetu, kuyapunguza au kuyaondoa makosa kama hayo," alisema Mgunda.

Kuhusu Balua na Chasambi, alisema amekaa nao na kuwaeleza namna ya kufunga bao gumu na jepesi, huku akiwataka kutolazimisha kufunga sehemu ambayo ni ngumu.

„Balua alipiga mpira kwenye eneo ambalo kipa yupo, Chasambi pamoja na kufunga, ile shauku ya kutaka kufunga zaidi ndiyo maana amefanya vile," alisema kocha huyo.



Washambuliaji wa Simba Queens; Aisha Mnunka (kushoto), Ruth Ingosi (katikati) na Jentrix Shikangwa wakishangilia bao katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Bunda Queens iliyochezwa wiki iliyopita. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Simba SC yambakiza Ayoub Lakred

INATOKA UK. 24

ewe kama ama atasaini au kama akiona haina maslahi kwake amepewa baraka zote za kwenda kupata changamoto nyingine huko aendako," kiliongeza chanzo hicho.

Kilisema pia usajili mpya wamekamilisha kuwapa mkataba wa miaka miwili, beki wa Coastal Union, Lameck Lawi huku safari ya kwaheri ikinukia kwa kiungo mshambuliaji, Saido Ntibazonkiza.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amekiri kufanya mazungumzo na baadhi ya wachezaji waliomaliza mkataba akiwamo Lakred.

"Kuhusu wachezaji waliomaliza mikataba yao, tunaendelea na mazungumzo ili kuhakikisha tunawabakiza, suala la kocha mchakato unaendelea kwa kufuata mapendekezo yetu ni aina gani ya mwalimu tunayemhitaji," alisema Ahmed.

Simba kwa sasa iko chini ya Juma Mgunda baada ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, kurejea kwao kutokana na matatizo ya kifamilia.



## Gamondi aanika siri

INATOKA UKURASA 24

no katika kila mchezo kitu kilichoongeza hamasa kwa wachezaji.

„Shabiki ni mchezaji wa 12, unapocheza mbele ya mashabiki na wakawaunga mkono kinaongeza kitu kwenye timu, tumekutana na hali hii kutoka kwa mashabiki wa Yanga, wamefanya kazi yao na niweke wazi wamechangia ubingwa huu," alisema Gamondi.

Azam FC iliyoko katika nafasi ya pili na Simba inayofuata, zimebakia katika vita ya kuwania kumaliza nyuma ya mabingwa Yanga na kujihakikishia tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Vita nyingine iliyoko ni ya kupambana kujinusuru na janga la kushuka daraja, hadi sasa huwezi kusema lolote kutokana na tofauti finyu ya pointi iliyopo katika timu zilizoko mkiani.

# Michezo

Jumatano Mei 15, 2024

Nipashe




Rooney awashutumu wachezaji Utd UK. 21




## Simba SC yambakiza Lakred

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inakuwa na kikosi imara kwenye msimu ujao, uongozi wa Simba umeanza mchakato wa kuhakikisha inambakisha kipa wake chaguo la kwanza, Ayoub Lakred, kwa kumpa mkataba mpya wa miaka miwili ya kuendelea kuitumikia klabu hiyo ya Msimbazi.

Mbali na Lakred, taarifa kutoka Simba zinasema mabosi wa timu hiyo pia wameweka wazi hakuna ofa rasmi kutoka katika timu yoyote kwa ajili ya kuhitaji huduma ya beki wao Mkongomani, Henock Inonga.

Lakred, nyota raia wa Morocco, alisaini mkataba wa mwaka mmoja ambao unafikia tamati mwisho wa msimu huu.

Taarifa zilizopatikana jana zinasema viongozi wamekamilisha mazungumzo na kipa huyo ataendelea kusalia Msimbazi baada ya kukubali kuongeza mkataba wa miaka miwili.

„Mambo yameenda vizuri kwa upande wa Lakred, viongozi wamefanya mazungumzo naye na ameridhia kubakia Simba, atasaini mkataba mpya wa miaka miwili wa kuitumikia klabu yetu," kilisema chanzo chetu.

Kuhusu Inonga, chanzo chetu kilisema bado beki huyo ataendelea kusalia Wekundu wa Msimbazi kwa sababu hakuna ofa iliyopelekwa ikihitaji huduma ya Mkongomani huyo.

"Kuna baadhi ya wachezaji ambao mikataba ilifikia tamati wameongezewa, akiwamo Kibu (Dennis) na Israel Mwenda tayari wameshasaini mkataba wa miaka miwili kila mmoja ili kuendelea kusalia ndani ya Simba.

Kuhusu Chama (Clatous), bado amewekewa ofa mezani jukumu iliyobakia ni mchezaji mwenye-

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi aanika siri ya ubingwa 2023/24

## ●●● Uongozi imara, kujituma na nidhamu ya wachezaji vyatajwa ndio...

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuipa Yanga taji la 30 la tatu mfululizo la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema uongozi imara ndani ya klabu hiyo ndio chachu kuu ya mafanikio yao.

Rasmi juzi ikiwa ugenini Yanga ilitangaza kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Mtibwa Sugar na kufikisha pointi 71 ambazo hazitafikiwa na timu nyingine yoyote zikiwa zimebakia mechi tatu kumaliza msimu.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi, alisema uongozi wa Yanga ulioko chini ya Rais Hersi Said, umekuwa imara na unafanya ‚mambo makubwa' katika kikosi hali iliyopelekea kupata matokeo mazuri msimu huu na kutangaza ubingwa kabla ya msimu haujamalizika.

**Kocha huyo raia wa Argentina alisema klabu kubwa ya soka ina hitaji uongozi imara ili kusimamia na kufanikisha malengo yao na hilo limetokea kwa Yanga ambapo uongozi umekuwa karibu na timu na kuhakikisha mambo yote muhimu yanapatikana.**

„Ubingwa huu sio tu wachezaji wameufanikisha, lakini pia nitoe pongezi kwa uongozi wa klabu yetu, wamekuwa karibu na timu, wamekuwa wakiendesha mambo kisasa zaidi na kufanikisha mafanikio haya," alisema Gamondi.

**NIDHAMU, KUJITUMA**

Kocha huyo alisema wachezaji wake wameonyesha ukomavu mkubwa na kufuata misingi imara iliyowafikisha katika mafanikio.

Alisema wachezaji wote wa Yanga wamekuwa na nidhamu ndani na nje ya uwanja pamoja na kujituma muda wote wanapokuwa uwanjani kwa ajili ya kusaka ushindi jambo lililowafikisha walipo sasa.

„Nidhamu, kujituma na kupambana muda wote uwanjani kwa wachezaji wangu hii pia ni sababu ya mafanikio haya, wachezaji wangu kila mmoja amefanya kazi yake vizuri, kila mchezaji anapopata nafasi anapambana kuipa ushindi timu, huwezi kuacha kuwasifia wachezaji," alisema Gamondi.

Alisema hakupata shida katika suala la nidhamu ya wachezaji, kila mmoja alifanya kazi yake vizuri kujituma kila alipopata nafasi yakucheza.

Pia kocha huyo alisema kikosi kipana chenye wachezaji wenye ubora walichonacho kimechangia kutwaa ubingwa wa msimu huu.

Gamondi alisema hata pale aliopokuwa akiwakosa baadhi ya wachezaji, waliopewa nafasi walikuwa wakionyesha kiwango kizuri na kutoonyesha utofauti.

„Viongozi walikuwa makini kwenye usajili, nimekuwa na wachezaji ambao uwezo wao ni mkubwa, kila aliyepata nafasi alionyesha kitu, kuwa na kikosi kipana kulinipa wigo wa kuchagua wachezaji wa kucheza kulingana na aina ya mechi," alisema Gamondi.

**MASHABIKI**

Kocha huyo aliendа mbali zaidi na kusema mashabiki wa klabu hiyo wanatakiwa kuwa sehemu ya mafanikio kwa sababu walionyesha upendo kwa timu yao na kuwaunga mko-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >